# Nipashe

Alhamisi Aprili 21, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580922

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US








**Padri** aliyekutwa amekufa mwili wake kuzikwa leo

UKURASA 4




# CAG: Fedha za mifuko hifadhi jamii hatarini

• **Anusa** hasara mabilioni kisa uwekezaji duni...*Endelea ukurasa 2*




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akipokea zawadi ya mfungo wa mwezi Ramadhani kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa Benki ya CRDB, Bruce Mwile, ofisini kwake, jijini Dodoma jana, ikiwa ni sehemu ya utamaduni wa Benki hiyo, kushirikiana na wateja na makundi mbalimbali ya jamii katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Uvunjaji nyumba, wizi vyombo kwenye magari sasa washika kasi

UKURASA 2

# Mwinyi ahimiza kufanyika siasa za kistaarabu, amani

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na wajumbe wa kikosi kazi cha Rais Samia Suluhu Hassan cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa Tanzania, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**


**MICHEZO** **SIMBA YAMBURUZA KOCHA ORLANDO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo kuhusu namna ya kudhibiti wadudu wanaodhuru waenezao magonjwa mbalimbali, alipotembelea moja ya Kiwanda kinachotengeneza viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti wadudu hao cha SC Johnson Family, katika mji wa Chicago, nchini Marekani juzi. Kushoto ni Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya SC Johnson Family, Dk. H. Fisk Johnson. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi asisitiza siasa za kistaarabu, amani

**Na Mwandishi Wetu**

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesisitiza umuhimu wa kufanya siasa za kistaarabu kwa kuweka mbele maslahi ya taifa na kudumisha amani.

Rais Dk. Mwinyi alitoa rai hiyo jana Ikulu Zanzibar alipofanya mazungumzo na Kikosi Kazi cha Rais Samia Suluhu Hassan cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kikiongozwa na Mwenyekiti wake, Prof. Rwekaza Mukandala.

Katika mazungumzo hayo, Rais Dk. Mwinyi alisema hakuna jambo kubwa katika Taifa lolote duniani isipokuwa amani, ambayo inakuja kwa kufanya siasa za kistaarabu.

Alimpongeza Rais Samia kwa kuunda kikosi kazi hicho ili kikusanye maoni na baadae kitoe mapendekezo kwa Serikali zote mbili nazo ziweze kuyafanyia kazi ili kuhakikisha nchi inadumu katika amani na siasa zinafanywa kistaarabu kwa maslahi ya nchi.

Alisisitiza haja kwa Watanzania wote kuunga mkono juhudi hizo hususan vyama vya siasa, hatua ambayo alisema itaondoa changamoto zilizopo.

Alikishukuru kikosi kazi hicho na kueleza haja ya kukamilisha kazi waliyoianza, huku akiahidi umma wa Watanzania na Wazanzibari wote kwamba mapendekezo yatakayoletwa na kikosi kazi hicho yatafanyiwa kazi ili kuondokana na changamoto za utendaji wa siasa nchini.

Aidha, alieleza haja kwa Kikosi Kazi hicho kuendelea kukaribisha maoni na kuyakusanya kwa lengo la kuyafanyia kazi ambapo kati ya maeneo tisa yaliyoelezwa na Kikosi Kazi hicho matatu kati yake bado yana changamoto zaidi ikiwemo Katiba Mpya, utaratibu wa uchaguzi na mikutano ya hadhara.

Rais Dk. Mwinyi aliviomba vyama vya siasa ambavyo havijaamua kuwa sehemu ya jambo hilo viamue kuingia kwa sababu lazima Watanzania wote wawe sehemu ya jambo hilo muhimu.

Alisema njia nzuri za kutatua changamoto ni kupitia katika mijadala kama hiyo badala ya kuyatumia majukwaa ya kisiasa na kuanza kutoa shutuma kwa wengine jambo ambalo halileti amani katika nchi.

Alikipongeza Kikosi Kazi hicho kwa kufanya kazi kwa uzalendo na kusisitiza kwamba maslahi ya nchi ni vyema yakawekwa mbele kuliko vyama vya siasa, kwani nchi ni muhimu zaidi kwa lengo la kupata amani na maendeleo.

Alieleza matumaini yake juu ya Kikosi hicho kutokana na mchanganyiko wa wajumbe wake, huku akieleza kwamba kutokana na migogoro inayojitokeza kila ikifika wakati wa uchaguzi Zanzibar basi ni vyema wadau wakubwa wa Kikosi Kazi hicho wakawa Wazanzibari pamoja na vyama vyote vya siasa Zanzibar ambavyo vitakuwa sehemu ya maoni hasa katika kuelekea uchaguzi wa mwaka 2025.

Alieleza kwamba si vyema kuona yale yaliyojitokeaza siku za nyuma yanajirejea kwani wakati huu ndio muafaka wa kueleza changamoto zilizopo na kuzifanyia kazi ili ifikapo mwaka 2025 mambo yote yawe yamewekwa vizuri ili kuingia katika uchaguzi kwa amani na usalma.

Alisema kwamba amani iliyopo hivi sasa haiwezi kudumu kama bado kuna baadhi ya maeneo ya huku na kule ambayo hayatowekwa sawa na kueleza haja ya kuwapo ushiriki kwa vyama vyote ili mambo yakae sawa kwani kazi hiyo ikikamilika itasaidia siasa nchini.

Akitoa taarifa ya Kikosi Kazi hicho, Prof. Mukandala alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa juhudi zake kubwa anazozifanya katika kuleta maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa hapa Zanzibar.

Alitoa shukrani kwa hotuba ya Rais Dk. Mwinyi ya ufunguzi ambayo ilitoa mwongozo wa kufanya siasa za kistaarabu, huku ikizingatiwa maslahi ya Taifa ikiwemo kudumisha amani, utulivu na umoja wa kitaifa.

# Uvunjaji, wizi majumbani Dar es Salaam washika kasi

**Na Romana Mallya**

MATUKIO ya kuvunja madirisha na milango kisha kuiba vitu vya thamani kwenye nyumba pamoja na magari katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Dar es Salaam yameanza kushika kasi.

Kutokana na hali hiyo, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limetoa rai kwa mitaa ambayo haina vikundi vya ulinzi shirikishi vianzishe ili kudhibiti matukio hayo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, waathirika wa matukio hayo walisema wahalifu hao wamekuwa wakitumia dawa za usingizi kupuliza vyumbani nyakati za usiku wakati watu wamelala ili kutekeleza uhalifu pasipo wahusika kugundua.

Mmoja wa waathirika wa tukio hilo, Mary Mashina, ambaye ni mkazi wa Tabata Segerea Chama, akisimulia alivyoibiwa alisema mwanzoni mwa Machi, mwaka huu, waliamka asubuhi na kukuta wameibiwa baadhi ya vitu vya ndani.

"Siku hiyo watu wote nyumbani tulichelewa kuamka. Tuliamka majira ya saa tatu asubuhi hali ambayo si ya kawaida. Nipoenda subuleni nikakuta televisheni na redio hakuna na mlango ukiwa umevunjwa. Nikabaini kwamba tumeibiwa. Nikaenda Kituo cha Polisi Stakishari kuripoti," alisema.

Mkazi mwingine wa Kimara Saranga, maarufu Kwa Makofia, Mayala Mwendesha, aliliambia gazeti hili kuwa juzi usiku aliibiwa gari lenye namba za usajili T 540 DVJ aina ya Probox Succeed lenye rangi ya silver.

Alisema wizi huo ulifanyika usiku baada ya kutoka safarini na familia yake, kisha kuliegesha gari nje kwamba alipoamka asubuhi hawakukuta gari.

"Nilipata msiba mama yangu alifariki dunia kwa hiyo nilisafiri pamoja na familia yangu kwa kutumia gari hilo ambalo ni mali ya mdogo wangu. Tumerudi nyumbani (Dar es Salaam) jana (juzi) na tulifika majira ya saa nne usiku.

"Ndani ya gari tulikuwa tumeweka vitu mbalimbali vikiwamo vyakula ambavyo tulinunua wakati tunarudi. Baada ya kufika nyumbani niliwaambia wanafamilia vitu hivyo watavishusha kesho (juzi) asubuhi maana wote tulikuwa tumechoka," alisema.

Alisema kitu ambacho alishuka nacho kwenye gari ni kompyuta mpakato na vingine viliendelea kubaki kwenye gari hilo.

"Ilipofika jana (juzi) asubuhi baada ya kuamka ndipo tulikuta gari halipo. Nyumba yangu imezungusha ukuta isipokuwa eneo la mbele pako wazi sijamaliza ujenzi. Nimetoa taarifa Kituo cha Polisi Gogoni Kiluvya," alisema.

Mkazi wa Tabata Kinyerezi Mtaa wa Zimbili (jina limehifadhiwa) alieleza Nipashe kuwa usiku wa kuamkia juzi, alisikia kelele kutoka nyumba ya jirani yake akiomba msaada baada ya kuvamiwa na wezi.

"Wakati jirani yangu akiomba msaada akiita wezi wezi, wale wezi wakatoka nje nikawa nawasikia wakiongea nje ya ukuta wa nyumba ninayoishi wakisema yeyote atakayesogea watamdhuru," alisema.

Alisema ilipofika asubuhi alibaini kwamba jirani yake aliibiwa televisheni na simu, kisha kujeruhiwa na panga mkononi.

Kijana huyo alisema kabla ya tukio hilo, wiki moja iliyopita mwanafunzi mmoja wa shule ya msingi wakati akieenda kituo cha daladala majira ya saa 12:00 alfajiri, alivamiwa na vibaka kisha kumpora begi lake na kukimbia nalo.

"Hawa vibaka ninadhani walijua ndani ya begi kuna kompyuta mpakato. Sasa wakati mtoto akipiga kelele za kuomba msaada, wale vibaka walipokimbia mbele walipekua na kukuta lina madaftari, hivyo walilitelekeza njiani," alisema.

Kutokana na kutokea kwa matukio hayo Nipashe ilimtafuta Kamanda Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, ambaye alikiri kwa baadhi ya maeneo ambayo hayana vikundi vya ulinzi shirikishi yamekuwa yakikumbwa na matukio hayo.

"Tabata Magengeni, Tabata Kimanga, Mwenge na maeneo mengine tumeshadhibiti. Walipiga kidogo miezi minne iliyopita lakini kwa sasa imebaki hadithi, kazi kubwa imefanyika. Baadhi ya maeneo wako vibaka lakini kazi kubwa inafanywa na Jeshi la Polisi ya kuwadhibiti," alisema.

Hivyo, alitoa wito kwa wananchi kuhakikisha maeneo ambayo hayana vikundi vya ulinzi shirikishi vianzishe ili kudhibiti uhalifu kama walivyofanya maeneo mengineyo.

# CAG abaini fedha mifuko hifadhi ya jamii ziko hatarini

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini mifuko ya hifadhi ya jamii iko hatarini kupata hasara ya mabilioni ya shilingi kutokana na utekelezaji duni wa miradi yake ya ubia na kampuni mbalimbali.



CAG Charles Kichere

CAG Charles Kichere anabainisha hayo kwenye ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Jumanne iliyopita, hivyo kuwa wazi kwa umma.

Anasema dosari ya kwanza ameibaini kwenye mradi wa Kiwanda cha Tangawizi cha Mamba Miamba, akifafanua kuwa mwaka 2016, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa LAPF (kwa sasa PSSSF) ulikubaliana na Chama cha Ushirika cha Wazalishaji wa Tangawizi cha Mamba-Miamba kufufua na kukifanya Kiwanda cha Tangawizi cha Mamba-Miamba katika Kijiji cha Mamba Miamba wilayani Same kuwa cha kisasa.

CAG anasema kiwanda hicho kilikuwa kimesimama kutokana na matatizo ya kiteknolojia na kwamba randama ya makubaliano kati ya Chama cha Ushirika cha Wazalishaji wa Tangawizi na LAPF iliyotiwa saini Septemba Mosi, 2020 ilieleza kuwa mfuko utamiliki hisa asilimia 67 na Chama cha Ushirika cha Mamba kitamiliki hisa asilimia 33.

Anasema kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, mfuko ulikuwa umetumia Sh. bilioni 1.71 kwa ajili ya kufufua kiwanda hicho na shughuli zingine za usimamizi.

Hata hivyo, CAG anasema alibaini kuwa hadi Novemba 2021, kiwanda kilikuwa hakijaanza uzalishaji kwa sababu ya kuchelewa kufunga mashine.

"Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma ulieleza kuwa kuchelewa kufungwa kwa mashine za kiwanda hicho kulisababishwa na kuchelewa kusafirisha mashine hizo kutoka kwa mtengenezaji nchini China kutokana kuzuka kwa janga la UVIKO-19 lililosababisha kuwekwa vizuizi vya usafirishaji," anasema.

**BIDHAA ZA TIBA**

CAG anaitaja dosari ya pili iliyoko kwenye mradi wa Kiwanda cha Bidhaa za Tiba cha Simiyu, akifafanua kuwa tarehe 11 Novemba 2016, Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Benki ya Uwekezaji - Maendeleo (TIB-Development), Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda (TIRDO), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba (TMDA) (zamani Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania-TFDA)walitia saini randama ya makubaliano ya kuanzisha kiwanda cha bidhaa za tiba zinazotokana na malighafi ya pamba katika Kijiji cha Dutwa, Bariadi.

CAG anasema kuwa kwa mujibu wa upembuzi yakinifu uliofanywa na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, gharama za mradi huo zilikuwa Sh. bilioni 69.21 zitakazogawanywa sawa baina ya wabia.

"Tarehe 13 Juni 2018, WCF na NHIF walisajili kampuni maalumu ya kuendesha kiwanda hicho. Ombi la idhini ya uanzishaji wa kiwanda liliwasilishwa kwa Wizara ya Fedha na Mipango tarehe 26 Juni 2019.

"Gharama hizi zilijumuisha gharama za awali ambazo ni pamoja na gharama za mikutano na gharama za upembuzi yakinifu," CAG Kichere anabainisha katika ripoti yake hiyo.

Anasema kuwa dosari nyingine iko kwenye mradi wa Kiwanda cha Chai cha Mponde, akifafanua kuwa mnamo mwezi Januari 2016, serikali ilijimilikisha Kiwanda cha Chai Mponde kutoka cha Wakulima wa Chai Samara (UTEGA) kilichobinafsishwa awali baada ya UTEGA kushindwa kukiendesha kiwanda hicho.

"Kupitia juhudi za Msajili wa Hazina, Septemba 2019, WCF na NHIF waliingia makubaliano ya kufufua Kiwanda cha Chai cha Mponde. Kwa mujibu wa upembuzi yakinifu, mtaji uliohitajika kufufua kiwanda ni Sh. bilioni 4.05 na hisa za kiwanda zingemilikiwa sawa baina ya wabia.

"Katika ukaguzi wangu, nilibaini serikali ilitoa kibali cha uendelezaji wa kiwanda mwezi Machi 2021. Hata hivyo, hadi Novemba 2021 kiwanda kilikuwa hakijaanza uzalishaji kutokana na kusubiri ununuzi wa mashine za kufufua kiwanda na ukarabati wa majengo na mifumo ya maji na umeme.

CAG ana angalizo kwamba kuchelewa kuanza kwa uzalishaji wa viwanda hivyo kunaathiri kufikiwa kwa malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) uliopangwa kuleta mageuzi ya uchumi kupitia viwanda.

"Ninapendekeza mifuko ikijumuisha PSSSF, WCF, NHIF na NSSF iharakishe kufungwa kwa mashine na kujenga miundombinu husika ili kuanza uzalishaji haraka katika viwanda vilivyoanzishwa au kununuliwa na mifuko hii, na serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itoe kibali cha kuendeleza Kiwanda cha vifaatiba cha Simiyu," anasema.

**USIMAMIZI DUNI**

CAG Kichere analitaja eneo lingine lenye dosari kwa mifuko hiyo kuwa ni usimamizi duni wa kampuni tanzu na kampuni za ubia zinazomilikiwa na mashirika ya umma.

Anasema amebaini ongezeko la mtaji lenye mgogoro katika Kituo cha Uwekezaji cha APC - Bunju, akifafanua kuwa Februari 2, 2015 Mfuko wa Pensheni wa GEPF (kwa sasa PSSSF) uliingia mkataba wa ubia na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) ya kukamilisha na kuendesha kituo hicho.

Anaendelea kubainisha kuwa makubaliano hayo yanaeleza kuwa, asilimia 80 ya faida inayopatikana inapaswa kugawanywa kwa wabia kulingana na umiliki wao na asilimia 20 ya faida iwekwe kama akiba ya kuendesha biashara.

"Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Sekta ya Umma ulikuwa umewekeza Sh. bilioni 9.93 ambazo ni asilimia 55.3 ya umiliki wakati NBAA imewekeza Sh. bilioni 8.02 ambayo ni sawa na asilimia 44.7.

"Kituo cha Uwekezaji cha APC kimekuwa kikipata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo iliyopita (2018/19-2020/21), na kwa mwaka wa fedha 2020/21 kituo kilipata hasara ya Sh. bilioni 2.35 (Sh. bilioni 5.17 mwaka 2019/20).

" Mwenendo huu wa hasara unaleta shaka ya kurejeshwa kwa kiasi kilichowekezwa na wabia. Nilibaini kuwa, NBAA ilikopa Sh. bilioni 15 kutoka (NSSF) ambazo zimedhaminiwa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Uwekezaji cha APC," anasema.

CAG anaendelea kubainisha kuwa kutokana na kituo kushindwa kulipa mkopo, NBAA iliomba mkopo huo kutambulika kama mtaji wa mfuko wa NSSF kwenye kituo hicho.

Hata hivyo, CAG anasema Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Sekta ya Umma ulikataa utaratibu huo kwa madai kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii wa Sekta Binafsi (NSSF) siyo sehemu ya wabia na pia haikuhusika katika kukopa endapo utaratibu huo utakubaliwa basi umiliki wa NBAA upungue kwa kiasi atakachopewa NSSF.

"Ninapendekeza PSSSF na NBAA waharakishe utatuzi wa mgogoro wa nyongeza ya mtaji ili wabia waweze kupata mapato stahiki yanayoendana na uwekezaji walioufanya," CAG anawasilisha hoja yake.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470DODOMA,
21.03.2022

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya **tarehe 19.04.2022 hadi 05.05.2022** kampuni ya Spedag Interfreight itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Holili kuelekea Moshi, gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW052Z / ZG3212**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - Mita 28.4 Upana - Mita 5.0 Kimo - Mita 5.6**

3. Njia itakayotumika: Holili hadi Moshi kupitia Soweto, gari litasafiri muda wa mchana tu ( **Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Padri aliyekutwa amekufa kuzikwa leo

**Na Jenifer Gilla**

MWILI wa Paroko wa Parokia ya Mbezi Mshikamano, Padri Francis Kangwa, unatarajiwa kuzikwa leo katika makaburi ya Pugu eneo ambalo mapadri wote wanazikwa.

Padri huyo alikutwa amefariki dunia ndani ya tangi kubwa la maji lililoko nyuma ya nyumba ya makazi ya mapadri Mtaa wa Sokoine katika jengo la Ottoman, jijini Dar es Salaam.

Taarifa zilizotolewa jana na Chansela wa Kanisa Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Padri Vincent Mpwaji, zilisema kulikuwa na misa ya mkesha na leo kutakuwa na misa ya maziko.

"Ratiba ya mazishi ni kuwa usiku wa leo (jana) kutakuwa na mkesha wa kumuaga katika kanisa lake (Parokia ya Mbezi Mshikamano), kisha kesho (leo) kutakuwa na misa pamoja na maziko katika makaburi ya mapadri Parokia ya Pugu," alisema

Alipoulizwa kama padre huyo atazikwa kwa taratibu za kanisa, hakuwa tayari kutoa majibu na kumtaka mwandishi aende kwenye mazishi atapata majibu.

Taarifa iliyotolewa juzi na Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, ilisema uchunguzi wa awali kwa kushirikiana na mamlaka zingine, ulionyesha dalili kuwa padri huyo ambaye ni raia wa Zambia anaweza kuwa amejiua.

Padri huyo alifika katika kanisa la Mtakatifu Joseph lililoko mtaa wa Sokoine Aprili 12, 2022 kwa ajili ya ibada maalum na baada ya ibada hiyo alikwenda kwenye makazi ya mapadri kujipumzisha lakini hakuonekana mpaka Aprili 15, alipokutwa amefariki dunia katika eneo hilo.

Taarifa hiyo ilisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi kubaini chanzo halisi kilichosababisha kifo cha Padri huyo.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Al- Hikma, Sheikh Nurdin Kishik, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa shukrani zake kwa Watanzania wote walioshiriki katika mashindano makubwa ya kuhifadhi Qur-aan Tukufu Afrika, yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa hivi karibuni. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Mashindano hayo, Salum Kiza. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mke atuhumiwa kuua mume akidai hakuwa chaguo lake

**Na Richard Makore,**
MWANZA

MKAZI wa Kijiji cha Iseresere Kata ya Majimoto wilayani Serengeti mkoani Mara, Happy Nyasumo (18), anadaiwa kumuua mume wake kwa kumkata shingo, kwa madai kwamba hakuwa chaguo lake.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya mashuhuda (majina yamehifadhiwa) walieleza kuwa wawili hao walifunga ndoa Machi 31, mwaka huu, lakini baada ya muda mfupi Happy alirudi nyumbani kwa wazazi wake waishio Kijiji cha Mosongo na kuomba mume wake arudishiwe mahari aliyolipa kwa madai kwamba hakuwa chaguo lake.

Mashuhuda walieleza kuwa ombi la mwanamke huyo lilikataliwa na wazazi wake na kutakiwa kurudi kwa mumewe, huku wakimwambia kwamba ndoa ni uvumilivu.

Walieleza kuwa baada ya mwanamke huyo (Happy) kurudi nyumbani kwake ndipo alitekeleza kitendo hicho cha kumuua mumewe, akieleza kwamba hakuwa chaguo lake.

Nipashe lilimtafuta Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mara, Ally Kitumbu, ambaye alisema hajapata taarifa za tukio hilo na kuahidi kulifuatilia.

Katika tukio lingine, mkazi wa Kijiji cha Kiagata wilayani Butiama mkoani Mara, Nyamhanga Chacha (30), anadaiwa kumuua mkewe, Matinde Nyagorwe (20), kwa kumkata na panga shingoni kwa madai kuwa amechelewa kumzalia mtoto.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mara, Ally Kitumbu amethibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Alisema tukio hilo lilitokea Aprili 18, mwaka huu katika Kijiji cha Gusuhi wilayani Serengeti mkoani Mara nyumbani kwa wazazi wa mwanamke huyo.

Alisema kabla ya mauaji hayo, kulikuwa na ugomvi wa muda mrefu ambao ulisababisha Matinde kukimbilia kwao.

Kamanda Kitumbi alisema siku ya tukio Nyamhanga alimfuata Matinde kwa wazazi wake na kumkata na panga shingoni na kusababisha umauti.

Aliwataka wananchi kutafuta suluhu ya matatizo yao kwa kuwashirikisha watu wengi ili kuyapatia ufumbuzi, badala ya kunyamaza nayo na kuamua kufanya mauaji kama hayo.

## Chongolo aagiza kurudiwa mchakato wa utoaji fomu CCM

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewaagiza makatibu wa chama hicho ngazi za wilaya kurudia mchakato wa utoaji fomu kwa wagombea katika mashina, baada ya kubaini baadhi ya wanachama kunyimwa fursa hiyo kwa makusudi.

Chongolo alitoa agizo hilo jana wakati akiwa kwenye ziara Mkoa wa Dar es Salaam na kuzungumza na Halmashauri Kuu za Wilaya ya Ubungo na Kinondoni.

Aliagiza mchakato huo urudiwe ili kuwapa fursa wanachama wenye dhamira njema ya kugombea waweze kuchukua fomu hizo.

"Kwa sasa chama kipo katika uchaguzi ngazi ya shina na katiba yetu inatoa fursa na haki kwa kila mwanachama kuchagua na kuchaguliwa, kitu ambacho kinanisikitisha, kuna baadhi ya maeneo wanachama wananyimwa fursa hii tena wananyimwa kwa makusudi.

"Kwa hapa Dar es Salaam kuna maeneo kama Tandika, Manzese, Kimara, baadhi ya makatibu wa matawi kwa sababu wana maslahi yao binafsi wanawanyima baadhi ya wanachama kuchukua fomu kwa kuwaambia fomu zimeisha na hawawapatii ili wawapitishe watu ambao wanafikiri watasimamia maslahi yao, hili ninalipiga marufuku."

Aliwaagiza makatibu wa wilaya zote na maeneo yote ambayo wamebaini kuna matatizo hayo mchakato huo urudiwe.

"Tunataka wale wote wenye dhamira ya kuchukua fomu wachukue bila kuwekewa vizuizi, hiki sio chama cha mtu, hiki sio chama cha maslahi binafsi, hiki chama ni cha wanachama, ni lazima tutende haki kwa kuwa katiba yetu ya CCM inatutaka tufanye hivyo," alisema.

Aliwakumbusha viongozi hao kuwa dhamana walizonazo hazijawapa haki ya kufanya uamuzi wa ubinafsi.

Pia, alikemea utaratibu wa baadhi ya viongozi wa matawi kushiriki kuingiza watu katika daftari la wanachama kinyume na utaratibu ili wawapigie kura katika uchaguzi ujao.

"Baadhi ya maeneo hapa Ubungo, Babati, Mbeya, sehemu ya Tabora, watu wamechukua kadi wanakwenda kuwapa watu ambao wanataka watumike kuwapigia kura, naagiza kwa makatibu wa wilaya vitabu vilivyokuwa vimehakikiwa ndiyo vitumike kwenye kupiga kura na sio vinginevyo," alisema.

Chongolo alisema watafuatilia na wakibaini kuna maeneo ambayo vitabu vilivyokuwa vimehakikiwa vimeongezwa majina wakurugenzi (makatibu) wa uchaguzi watawajibika.

Alisema ni haki ya vijana nchini kuingia kwenye siasa kugombea na kuongoza na kutoa mchango wao kwa nchi.

Pia, aliwakumbusha vijana kuwa mwaka huu ni wa uchaguzi na kwamba hawakuzaliwa kuwa wa hamasa.

"Wito wangu kwenu vijana wote nchini, acheni kubakia kuwa wapambe tu wa wagombea na mkiona kuna mazingira ambayo yanataka kuwafungia milango tuambieni haraka tuna funguo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James, alisema miradi yote inayotekelezwa wilayani kwake inaendelea vizuri na inaridhisha, akitolea mfano upanuzi wa Barabara ya Morogoro.

# TET yawafunda walimu wa masomo ya ufundi

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Elimu Tanzania (TET), imeendesha mafunzo kazini kwa walimu wa masomo ya ufundi katika shule za sekondari za serikali na binafsi katika mikoa 10 ya Tanzania Bara na Zanzibar, mkoani Tanga.

Akifungua mafunzo hayo ya siku tano, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis, alisema mafunzo hayo yamelenga kuboresha utaalamu wa walimu na kuwezesha kujifunza masomo ya michepuo ya Ufundi, Biashara, Kilimo na Maarifa ya nyumbani.

"Napenda niwakumbushe kupitia kwenu taifa linatarajia kupata wahitimu waliobobea na wanaoweza kujiajiri au kuajiriwa katika fani mbalimbali ikiwamo ufundi mitambo, umeme na vifaa vya mawasiliano na ujenzi. Vile vile, tunaratajia wanafunzi wenu wakiandaliwa vizuri wataweza kujiajiri na kutengeneza ajira kwa watu wengine na matarajio haya hayatafikiwa endapo ufundishaji na ujifunzaji wa masomo haya hautalenga kumjengea mwanafunzi mwelekeo wa kutenda."

"Malengo hayo yakifikiwa, taifa litaweza kuendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia kwa kuwa litakuwa na vijana wenye uwezo wa kutumia maarifa ya ufundi katika kufikiri, kubuni na kuunda vifaa na nyenzo za kurahisisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwani kwa ujumla mafunzo haya pia yamedhamiria katika kukuza stadi za karne ya 21 ambazo ni mawasiliano, ushirikiano, ubunifu na fikra tunduizi," alisema.

Alisema serikali inaendelea kufanya jitihada za kutoa mafunzo mbalimbali kwa walimu ili kuboresha taaluma na utaalamu wao katika masomo mbalimbali yakiwamo ya ufundi.

Kwa upande wa Zanzibar, alisema uchumi wa buluu ni fursa na serikali imedhamiria kuwekeza kwenye miradi kadhaa mikubwa na midogo ya kiuchumi kwa wazawa na wageni katika uvuvi wa samaki, kilimo cha mwani, miundombinu ya uvuvi na usafirishaji wa mazao ya baharini yanayosafirishwa katika kiwango cha kimataifa na kwamba serikali inahitaji kuwa na vijana wengi wenye ujuzi wa kutosha katika uchumi wa buluu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TET, Dk. Aneth Komba, alisema mafunzo hayo yamefadhiliwa na serikali kwa asilimia 100 kupitia fedha za maendeleo zilizotolewa kwa TET na kwa mwaka wa fedha 2021/22 taasisi hiyo imepokea Sh. bilioni 1.24 huku akiainisha lengo la mafunzo hayo kuwa ni kuboresha mihtasari.

"Matokeo ya mafunzo haya tunatarajia walimu watatumia mbinu bora za ufundishaji wa masomo haya na hatimaye kumwezesha mhitimu kupata maarifa, stadi za kutenda na uelekeo wa kujitegemea kwa manufaa mapana ya jamii na taifa kwa ujumla," alisema.

Naye Mkurugenzi Msaidizi, Elimu ya Sekondari, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Hadija Mcheka, aliwataka washiriki kuyatumia mafunzo hayo waliyopata kwa ufasaha kwa kuchangia na wenzao waliowaacha vituoni kwa kuwa serikali inatarajia wataenda kuyasambaza na kutumia kwa wanafunzi walioko shuleni.




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru (katikati), akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari, jijini humo jana, kuhusu kuwaondoa kwa muda wafanyabiashara wa soko la Sabasaba, ili kupisha ujenzi unaotarajiwa kuanza mwezi Julai mwaka huu. Kulia ni Mweka Hazina wa Jiji hilo, Rahabu Philip na Ofisa Biashara wa Jiji, Donatila Vedasto. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri ataka hatua askari aliyeua mwanakijiji mgodini

**Na Mwandishi Wetu,**

DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuph Masauni, ameagiza hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya askari polisi aliyemuua mwanakijiji Cosmas Hamis (23) kwenye mgodi wa almasi wa El Hilali wilayani Kishapu mkoani Shinyanga mwezi uliopita.

Aprili 3 mwaka huu, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu mauaji dhidi ya kijana huyo aliyedaiwa kupigwa risasi pajani na mmoja wa askari polisi waliokuwa wanalinda mgodi huo mwaka huu.

Waziri Masauni akizungumza na Nipashe kwenye viwanja vya Bunge jijini hapa jana, aliagiza kufanyike uchunguzi kuhusu tukio hilo ili hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi ya askari aliyefanya mauaji hayo.

"Kwenye PGO (Kanuni za Mwongozo wa Utendaji wa Jeshi) kumeelekezwa hatua za kufuatwa wakati wa kutekeleza ukamataji wa watuhumiwa. Matumizi ya silaha ni hatua ya mwisho kabisa baada ya mbinu zingine kushindikana.

"Katika hili la mauaji ya mgodini, kuna haja ufanyike uchunguzi ili hatua zichukuliwe dhidi ya askari aliyehusika na mauaji hayo," Waziri Masauni aliagiza.

**UPELELEZI POLISI**

Nipashe ilipozungumza na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi George Kyando, Machi 25 mwaka huu, alikiri kuwapo kwa tukio la mauaji dhidi ya kijana Cosmas lakini akasita kulizungumzia kwa kina kwa maelezo kwamba lilikuwa kwenye uchunguzi wa vyombo vya dola.

Baada ya kauli ya Waziri Masauni jana, Nipashe ilirejea kwa Kamanda Kyando kujua mustakabali wa tukio hilo, alisema upelelezi unaendelea na ukikamilika wahusika watachukuliwa hatua.

Hata hivyo, Kamanda Kyando hakutaja majina wala idadi ya askari polisi wanaochunguzwa kuhusiana na tukio hilo, pia hakuweka bayana hatua za awali zilizochukuliwa dhidi yao, ikiwamo kusimamishwa kazi kupisha uchunguzi.

**KAULI YA LHRC**

Alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, Wakili Joyce Komanya, Ofisa Mipango Mwandamizi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) anayeshughulika na haki, uwajibikaji na mazingira, alimpongeza Waziri Masauni kwa kuagiza hatua zichuliwe dhidi ya aliyefanya mauaji hayo.

Hata hivyo, Wakili Joyce alitilia shaka ufanisi katika uchunguzi huo kwa kuwa unafanywa na polisi dhidi ya askari polisi, hivyo kuwapo mgongano wa kimaslahi. "Kinachotakiwa ni kuwa na chombo huru kitakachokuwa kinafanya uchunguzi dhidi ya askari polisi wanapokuwa na tuhuma za kukiuka misingi ya sheria na haki za binadamu.

"Uamuzi wa waziri ni mzuri lakini shida ipo kwenye nani anakwenda kuwachunguza polisi? Jibu ni kwamba polisi wanajichunguza wenyewe," Wakili Joyce alisema.

# Bashungwa amsimamisha kazi DED

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, imemsimamisha kazi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro, Hassan Njama, ili kupisha uchunguzi kwa kushindwa kutekeleza maagizo aliyoyatoa kwake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya TAMISEMI na Nteghenjwa Hosseah, Bashungwa amemsimamisha kazi mkurugenzi huyo kuanzia siku hiyo (jana).

"Waziri Bashungwa amechukua hatua hiyo baada ya Mkurugenzi huyu kushindwa kutekeleza maagizo aliyotoa wakati wa ziara yake ya kikazi aliyoifanya Machi 17, mwaka huu kwenye halmashauri hiyo," alisema.

Taarifa hiyo ilisema wakati wa ziara ya waziri huyo alibaini upotevu wa fedha za miradi na matumizi yasiyo sahihi ya Sh. milioni 231.84 katika ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kumbukumbu ya Moringe Sokoine.

"Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa bwalo la chakula, jiko na bweni na kumuagiza mkurugenzi huyo kuwachukulia hatua za kiutumishi wakuu wote wa idara na watumishi waliohusika na ukiukwaji wa taratibu za matumizi katika mradi huo."

Taarifa hiyo ilisema hadi kufikia jana hakuna mkuu wa idara yoyote ama mtumishi aliyechukuliwa hatua kutokana na agizo hilo.

Kutokana na hilo, Waziri Bashungwa ameendelea kuwataka wakurugenzi wa halmashauri zote kuendelea kusimamia miradi ya maendeleo kikamilifu na kuchukua hatua za haraka pale wanapobaini ubadhirifu wa fedha za umma.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Halmashauri ziwapange machinga

**HIVI** karibuni askari mgambo wa Jiji la Mwanza, walimwaga matunda ya machinga aliyekuwa anafanya biashara ya kubeba matunda kichwani na kumsababishia hasara kubwa.

Tayari Jiji la Mwanza limechukua hatua baada ya Waziri Ofisi Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, kuwaonya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Mwanza, kujitafakari dhidi ya tukio hilo.

Tukio hili linakumbusha enzi za mgambo wa maeneo mbalimbali ya majiji walivyokuwa wanamwaga bidhaa na vyakula vya wafanyabiashara wadogo waliokuwa wanajitafutia riziki kwenye maeneo mbalimbali.

Tukio hili ni la unyanyasaji na ni ukatili mkubwa kwa watu wadogo wanaojitafutia riziki, kwa kuwa kuna uwezekano wa kutafuta maeneo ya kuwapanga, lakini aliyebeba matunda yake kichwani anakuwa kero ipi kwa watumiaji wengine?

Kuna wakati yalitolewa maelekezo ya kutowabugudhi wafanyabiashara hao, hali iliyosababisha kujaa kila mahali kiasi cha kuchafua mji, maeneo ya barabara yaliyotengwa kwa watembea kwa miguu kutoonekana, huku wakijaa kwenye vituo vya daladala jambo lililosababisha kero kwa wafanyabiashara.

Kutokana na hali hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan, aliagiza wakuu wa wilaya, halmashauri kuwapanga wafanyabiashara hao kwa kuwatafutia maeneo maalum, kuwaondoa kwenye maeneo yasiyofaa na kuwapeleka kunakostahili ili kuweka utaratibu kwenye mitaa mbalimbali.

Katika kuwapanga inapaswa halmashauri kuweka utaratibu mzuri ambao hautawaumiza na sio kukimbizana nao mtaani na kuharibu mali zao, bali kuhakikisha wanakwenda kule kunakostahili kwa kutoa elimu ya mara kwa mara na kuweka mabango.

Mathalani, kwa Dar es Salaam, machinga wamerejea kwenye maeneo waliyoondolewa na kumekuwa na malalamiko ya kuwapo rushwa ili waruhusiwe kubakia kwenye eneo husika, jambo linalosababisha mgongano kwa kuwa wanapokuja wengine ambao hawapo kwenye utaratibu huo wanaondolewa kwa nguvu.

Kuongezeka kwa wafanyabiashara wadogo mtaani ni dhahiri kuwa tatizo la ajira ni kubwa, lakini halmashauri hazijaweka utaratibu mzuri wa kutoa elimu ya biashara na matumizi sahihi ya mikopo ya asilimia 20 kwa ajili ya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Kuruhusu mgambo wafukuzane na wamachinga mtaani ni kukaribisha rushwa kama inavyolalamikiwa sasa kwenye maeneo mengi ya jiji hasa Kariakoo, au kusababisha madhara ya mali na mwili kwa wanaofanya biashara.

Ni lazima kufuatilia na kuboresha mazingira ili waendelee kufanya biashara kwenye maeneo husika, kuhakikisha wanakusanya kodi kutoka kwao na kuchangia maendeleo ya nchi.

Ni muhimu mgambo kuelezwa mipaka ya kazi yao, lakini kuepuka kuhangaika na vitu vidogo ambavyo wakati mwingine havina madhara, mfano muuza matunda anayeuza akiwa amebeba kwenye beseni, anaathiri vipi mazingira, wakati uchafu anabaki nao kwenye beseni lake.


Machinga wanaohitaji kupangwa kwenye maeneo maalum ni wenye viduka vidogo na vibanda, ambao wengi hawalipi kodi huku baadhi ya wafanyabiashara wakiondoka kwenye utaratibu wa kulipa kodi jambo ambalo linainyima serikali mapato.

Muhimu sana kwa halmashauri kufuatilia kwa karibu maeneo walikowapeleka kama wameenda au wamebaki kwenye maeneo ya zamani, lakini kujua kwanini hawaendi na kushughulikia changamoto zilizopo.

Ni muhimu kwa serikali kuendeleza maeneo ya vijijini ili kuwafanya wahamaji kubaki huko kufanya shughuli za kujipatia kipato, mtu anapokuwa na uhakika wa kuingiza kipato kwenye eneo alilopo hana haja ya kukimbilia mjini.

Lazima kuhakikisha maendeleo yanakuwapo vijijini, barabara, maji na umeme vinapatikana, ili mtu aweze kusafirisha bidhaa na mazao yake kuyafikia masoko kwa urahisi kuuza na kununua, hali ambayo itamwezesha kupata kipato cha kukidhi mahitaji ya msingi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Pandisheni nauli, lakini msituumize abiria

Na Adam Fungamwango

**KUTOKANA** na vita inayoendelea kati ya Russia dhidi ya Ukraine, bei ya mafuta imeshaanza kupanda si Tanzania bali duniani kote.

Tayari baadhi ya mikoa ya pembezoni mwa nchi kama Katavi, Kigoma, ina semekana bei imeshaanza kupanda. Mafuta yakipanda, mara nyingi mfumuko wa bei hauepukiki.

Wakati hali ikiwa hivyo tumesikia Wamiliki wa Mabasi Nchini Tanzania pamoja na Mamlaka ya Usafiri Ardhini Nchini (LATRA) wakiwa kwenye mchakato wa kutaka kupandisha nauli kutokana na gharama za uendeshaji kupanda, ikiwemo bei ya mafuta.

Kwa jinsi tunavyosikia na hali ilivyo sasa duniani, ni ngumu sana kukataa eti nauli zisipande, kwani huko ni kujidanganya.

Vita imesababisha kupungua hata meli za mafuta kuja nchini, lakini hata huko pia uzalishaji umepungua kutokana na tatizo hilo hilo.

Tunatarajia nauli itapanda, hilo wala halina mjadala kwa sababu hata baadhi ya bidhaa mitaani zimeshaanza kupanda.

Kupandisha nauli kutawafanya wamiliki hao kuweza kumudu gharama za kuendesha na kulinda mabasi yao, si kuweza kuweka mafuta tu, pia kuyafanyia matengenezo ili yawe salama kwa abiria na kuwafanya wasafiri kwa raha.

Pia, wamiliki wataweza kuendelea kupata pesa za kuwalipa madereva, makonda, wakata tiketi, mafundi na wafanyakazi wote wa mabasi hayo na wao kupata faida itakayowawezesha kuendelea kuifanya biashara hiyo ya kusafirisha abiria.

Hata hivyo, chonde chonde tunawaomba kuangalia pia hali za Watanzania kwa sasa jinsi zilivyo.

Wakati wa vikao hivyo vya kupanga bei, waangalie jinsi Wabongo 'walivyochoka', hivyo bei watakayopandisha iwe rafiki na isiwaumize.

Kuna bei ambazo ukipandisha unaweza kufukuza wateja, wakabaki nusu, lakini inawezekana kabisa mtu akapandisha bei ikaendelea kuwa rafiki kwa wateja na akapata faida kutokana na ule wingi wao kila wanapohitaji bidhaa.

Mfano ni kwamba sehemu nyingi za jiji la Dar es Salaam, nauli ni Sh. 400 na zile za maeneo ya mbali hadi 1000, kwani kwa sasa jiji la Dar es Salaam limepanuka sana, nauli inakuwa kuanzia Sh. 500, na kuendelea hadi hata kufikia Sh. 1,000.

Kama maeneo haya yote ikapandishwa shilingi mia moja, yaani maeneo ambayo daladala zilikuwa zikichukua abiria kwa Sh. 400, ikawa Sh. 500, na Sh 700, ikawa Sh 800, itakuwa ahueni kwa abiria.

Hata kwenye mabasi ya mikoani, kama ikiongezwa Sh. 1000 hadi 2,000 juu ya bei ya awali kutegemea na daraja la basi lenyewe, si mbaya. Mfano kama nauli ya kwenda mkoa fulani ni Sh 20,000, basi ipandishwe angalau iwe Sh 21,000.

Kama nauli itapanda hivi sidhani kama kuna abiria atahisi maumivu au kuathirika na namna yoyote ile kwa kupanda bei, lakini vinginevyo itakuwa ni kumpa mzigo mkubwa Mtanzania.

Hatutaraji sehemu ambayo abiria wanakwenda kwa Sh. 30,000, basi ipandishwe hadi Sh 40,000 hadi Sh 45,000.

Bei kama hizi si rafiki kwa Mtanzania, kwa sababu tayari huko alikotoka anakuwa amekutana na changamoto nyingine nyingi za kununua bidhaa ambazo nazo zimepandishwa.

Lakini, hili hata kwa baadhi ya wafanyabiashara wenye uzoefu na mambo hayo wanajua kuwa ni bora kupandisha bei kidogo ili kuendelea kupata wateja wengi kwa sababu ule wingi wao unaziba lile pengo, kuliko kupandisha sana na kushindwa kupata wateja wengi, kwani badala ya kupata faida, sasa inakuwa ni hasara.

Kuna Watanzania wengi, mfano wakazi wa Dar es Salaam kwa sasa wanaishi mbali sana kutoka katikati ya jiji, kama Goba, Mpiji Magoe, Buza, Kisemvule, Chanika, Chamazi, Boko, Bunju, na sehemu nyingi ambazo zipo mbali na katikati ya jiji kama Kariakoo, Posta, Stesheni na maeneo ya karibu na hayo ambapo mara nyingi ndiyo huenda kutafuta riziki zao.

Hawa kwa kiasi kikubwa ndiyo watakaoathirika zaidi kama bei kubwa zitapadishwa, kwa sababu kwanza mpaka sasa tu nauli wanazotumia ni kubwa mno kwenda na kurudi kwenye usafiri, halafu kuna baadhi hadi wafike majumbani kwao, ni lazima pia wapande bodaboda ambazo nazo nadhani zitakuwa zimepandisha nauli zao.

Hawa ndiyo wa kuhurumiwa zaidi kwa sababu hata iweje, hawawezi kuamua kutembea kwa miguu kwenda kazini na kurudi majumbani, tofauti na wale wa Tandale, Kigogo, Mburahati, Mwananyamala, Kinondoni, Magomeni ambao wenyewe wakiamua wanaweza kuutwanga kwa mguu kwenda kazini kama ni katikati ya jiji.

# Mgambo watuhumiwa kukata watu mapanga

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamelalamikia vitendo vinavyofanywa na baadhi ya mgambo wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wilayani humo wanaodaiwa kuwakata mapanga wananchi wanaowakamata wakiwa na mazao ya misitu.

Diwani wa kata ya Iyenye, Lukas Makurumo, alibainisha hayo jana katika kikao cha Baraza la Madiwani cha halmashauri hiyo.

Alisema wamechoshwa na vitendo vinavyofanywa na mgambo hao vya kuwapiga na kuwajeruhi wananchi hususani wanapokuwa kwenye misako yao jambo ambalo linazua taharuki kwenye jamii

Alisema Aprili 6, mwaka huu kwenye kata yake mtu mmoja alijeruhiwa kwa kupigwa na kukatwa mapanga na mgambo hao nyakati za usiku na mtu huyo mpaka sasa amelazwa hospitali akiendelea na matibabu na taarifa hizo waliziwasilisha ofisi za TFS. Alisema serikali inapaswa kuingilia kati suala hilo na kulitafutia ufumbuzi wa haraka kwa kuwa linaweza kusababisha kuvunjika kwa hali ya usalama.

Diwani mwingine wa Kata ya Muhongolo, Michael Mizubo alisema, mgambo hao wamekuwa wakiwakamata wananchi wakiwa wameficha sura zao kwa kuvaa soksi nyeusi ili kuficha sura zao wasitambulike hali ambayo inaleta hofu kwa wananchi.

Naye Mkuu wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Kahama, Rockius Mulokozi, alisema tukio la Aprili 6, mwaka huu, alipigiwa simu na diwani wa kata ya Iyenye kuhusu mgambo kuvamia wananchi na kuwacharanga mapamga na kwamba baada ya tarifa hiyo alituma askari wake na kwenda kutuliza vurugu zilizokuwa zikiendelea. Akijibu malalamiko hayo Meneja wa TFS, Ester Josephati alisema, taarifa ya wananchi kupigwa na mgambo wanazo na wameanza kufuatilia sakata hilo kwa ukaribu ili kuhakikisha kila aliyehusika anachukuliwa hatua za kisheria na kwamba mgambo wao hawafanyi kazi kwa kuficha sura zao.

Hata hivyo, Josephati aliwataka madiwani hao kuamini kuwa TFS ipo kwa ajili ya



Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo Mathew (kushoto), akifurahia jambo na Balozi wa China hapa nchini, Chen Mingjia, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Lugha ya Kichina Duniani, katika ofizi za ubalozi, jijini Dar es Salaam juzi jioni. **PICHA: UBALOZI WA CHINA**

# Mbaroni tuhuma kuua kwa jembe

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia Kashue Ndhovu (18), mkazi wa kijiji cha Nyakaiga wilayani Karagwe, Mkoa wa Kagera , kwa tuhuma za kumuua kwa kumkata kwa jembe kichwani Thomas Paulinus (25), mkazi wa kijiji hicho.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani humo ACP Maketi Msangi alisema kuwa mtuhumiwa huyo anadaiwa kumkata mwanakijiji mwenzake baada ya kugoma kushirikiana na wananchi wenzake katika kazi za maendeleo wakati wa kujenga barabara ya kitongoji cha Kishasha, Aprili 15, 2022.

"Mtuhumiwa alimkata Thomas katikati ya kichwa kwa jembe, akasababisha damu kuvilia kwenye ubongo, hali iliyosababisha kifo chake wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Nyakahanga, iliyoko katika wilaya ya Karagwe," alisema.

Msangi alisema kuwa Thomas alifariki siku ya tukio na kwamba mtuhumiwa huyo atafikishwa mahakamani wakati wowote baada ya upelelezi kukamilika.

Katika tukio jingine, alisema wanawashikilia watuhumiwa watatu kwa tuhuma za kupatikana na dawa za kulevya aina ya mirungi gomba/pakiti 485 yenye uzito wa kilogramu 39.

Aliwataja wanaoshikiliwa ni Jairu Salimu (33), Mustapha Rashid (53), wakazi wa Manispaa ya Bukoba na Medard Kahamba (48), mkazi wa Kanyigo Wilaya ya Missenyi.

Alisema kuwa watu hao walikamatwa Aprili 18 mwaka huu saa 4:00 asubuhi katika Kata ya Kanyigo wilayani Missenyi, wakiwa kwenye usafiri wa pikipiki mbili aina ya Bajaj Boxer zenye namba za usajili MC 421 CSZ na MC 544 CXZ, wakielekea Bukoba.

" Baada ya kukamatwa na kukaguliwa, walibainika kuwa wamebeba mirungi ambayo ilifungwa katika mifuko ya sandarusi, upelelezi unaendelea baada ya kukamilika tutawafikisha mahakamani." alisema Msangi.

# Maelfu ya Watanzania wajifunza Kichina

**Na Mwandishi Wetu**

IDADI ya Watanzania wanaojifunza lugha ya Kichina katika taasisi zinazofundisha lugha hiyo, kwenye vyou vikuu vya Dar es Salaam (UDSM) na Dodoma (UDOM) imezidi kuongezeka na hadi sasa wamefikia 20,000.

Balozi wa China nchini Tanzania, Chen, alibainisha hayo juzi katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Lugha ya Kichina kwa mwaka 2022, yaliyofanyika katika ubalozi wa China, Dar es Salaam.

Chen alisema hatua hiyo inaonyesha shauku kubwa waliyo nayo vijana wengi wa Tanzania katika kujifunza lugha hiyo ambayo ni moja ya zile zinazotumika katika shughuli mbalimbali kimataifa ikiwamo katika Umoja wa Mataifa.

"Wanafunzi wengi wa Tanzania wana mipango ya kusoma nchini China siku zijazo na kwamba hayo ni matokeo ya ushirikiano kati ya China na Tanzania katika sekta ya elimu. Tunatarajia kuona vijana wengi zaidi wa Tanzania wakijifunza na kumudu lugha ya Kichina," alisema.

Maadhimisho hayo yalikuwa na kaulimbiu: "Kujifunza Lugha ya Kichina na kujenga pamoja mustakabali mwema kwa Tanzania na China." Naibu Waziri wa Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Mhandisi Kundo Mathew, katika hotuba yake alirejea kumbukumbu zake alipokuwa akisoma katika Chuo Kikuu cha Hunan miaka kadhaa iliyopita akielezea umuhimu wa lugha ya Kichina.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, lugha hiyo ina ukaribu mkubwa na utamaduni na kwamba kujifunza Kichina kunaweza kuunganisha tofauti za kiutamaduni na kuendeleza maelewano baina ya watu kutoka nchi tofauti.

Alisisitiza kuwa kutokana na kasi ya maendeleo nchini China, lugha ya Kichina imeendelea kuwa maarufu duniani.

"Kwa sasa kuna kampuni nyingi zinazofanya shughuli nchini Tanzania na zimetoa ajira nyingi na maendeleo kwa vijana wa Kitanzania wanaojifunza lugha ya Kichina," alisema.

Katika hafla hiyo, wanafunzi wa Kitanzania walisomea lugha ya Kichina walionyesha umahiri wao kwa kushiriki michezo mbalimbali kwa lugha na utamaduni wa Kichina.

Wanafunzi hao na wale waliohitimu masomo ya lugha ya Kichina katika taasisi zinazofundisha lugha hiyo nchini, waliimba nyimbo za Kichina, kucheza Kung Fu na kushiriki katika mijadala na maigizo, hivyo kuwafanya waliohudhuria hafla hiyo kuburudika ipasavyo.

Siku ya Kimataifa ya Lugha ya Kichina iliandaliwa na Ubalozi wa China nchini kwa kushirikiana na Kituo cha Utamaduni cha China Tanzania na Taasisi ya Lugha ya Kichina katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mbali na Naibu Waziri Kundo, wengine waliohudhuria hafla hiyo ni Ofisa wa masuala ya Utamaduni na Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni cha China Tanzania, Wang Siping, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Prof. Bernadeta Killian na Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Charles Msonde.

# Asilimia 94 hatarini kuambukizwa malaria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASILIMIA 94 ya watu nchini wapo kwenye hatari ya kuambukizwa malaria ndani ya mwaka, huku utafiti ukionesha vifo vimepungua kwa asilimia 70.

Hata hivyo, serikali inatekeleza afua nne za kupambana na mbu wanaoambukiza ugonjwa huo na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa tiba, vitendanishi na dawa kwa zaidi ya asilimia 90 katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

Mkuu wa Kitengo cha ufuatiliaji wa tathmini ya udhibiti wa Malaria, Dk. Sijenunu Aron, aliyasema hayo alipokuwa akitoa mada ya hali ya maralia nchini katika semina kwa waandishi wa habari kuelekea maadhimisho ya siku hiyo ambayo hufanyika kila mwaka Aprili 25, duniani.

Alisema takwimu za dunia za mwaka 2021, zinaonesha kuwa kwa mwaka 2020 kulikuwa na ongezeko la wagonjwa wanaokadiriwa kufikia milioni 241 katika nchi 85 zenye ugonjwa huo kutoka wagonjwa milioni 227 huku vifo vikiongezeka hadi kufikia vifo 627,000 kukiwa na ongezeko la vifo 69,000 sawa na asilimia 12 ikilinganishwa na vifo 558,000 kwa mwaka 2019.

"Inakadiriwa vifo 47,000 sawa na asilimia 68 ya vifo 69,000 vilivyoongezeka vimechangiwa na uwapo wa ugonjwa wa Covid-19," alisema.

Kwa upande wa Tanzania, Dk. Aron alisema pamoja na kupunguwa kwa malaria hadi kufikia asilimia 7.5 mwaka 2017, bado asilimia 94 ya Watanzania wako katika hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa huo.

Alisema utafiti unaonesha kuwa maambukizi kwa watoto wa shule za msingi yamepungua kutoka asilimia 21.6 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 11.2 mwaka 2021.

Dk. Aron alisema idadi ya wagonjwa imepungua kwa asilimia 53 kwa kila wagonjwa 1000 kutoka 162 hadi kufikia wagonjwa 76.

Alisema mikoa ambayo ina kiwango kikubwa cha Malaria ni Lindi, Mtwara, Pwani, Ruvuma, Tanga na Tabora wakati ile yenye kiwango kidogo ni Kilimanjaro, Manyara, Arusha, Dodoma, Iringa, Singida na Njombe.

Dk. Aron alisema wagonjwa waliolazwa kutokana na Malaria imepungua kwa asilimia 32 kutoka wagonjwa 307,588 mwaka 2017 hadi 209,888 mwaka 2021 wakati vifo vimepungua kwa asilimia 70 kati ya vifo 100,000 kutoka vifo 6,311 mwaka 2015 hadi 1,909 mwaka 2021.

Alisema upatikanaji wa vifaa, vitendanishi na dawa katika vituo vya kutolea huduma umeongezeka kwa asilimia 97 mwaka 2021.



Mkurugenzi wa Sos Children Villages Tanzania, David Mulongo (katikati), akifungua kikao cha wamiliki wa vituo vya kulelea watoto, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa James Foundation, James Yustar na Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Mdathiru Makora. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rais Samia mgeni rasmi sherehe za Muungano

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye sherehe za miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zitazofanyika Aprili 26, 2022 ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete, Dodoma (Jakaya Kikwete Convention Centre).

Katika sherehe za maadhimisho hayo mwaka huu hakutakuwa na maonyesho ya gwaride la vikosi vya majeshi ya ulinzi na usalama kama ilivyo kawaida.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, George Simbachwene, akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana kuhusu maandalizi ya sherehe hiyo, alisema maandalizi yanaendelea vizuri.

=Alisema kutakuwa na uzinduzi wa andiko la historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kongamano litakalowashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo viongozi waliopo madarakani na wastaafu, wanasiasa mbalimbali, wanazuoni na wanafunzi wa vyuo vikuu pamoja na wananchi kutoka Tanzania na Zanzibar.

Alisema kwa kushirikiana na TAMISEMI kwenye sherehe hizo shughuli zingine zitakazofanyika ni pamoja na mashindano ya insha kwa wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari nchi nzima (Tanzania Bara na Zanzibar).

"Kamati ya wataalamu imeomba ridhaa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maadhimisho na Sherehe Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa Mikoa, Taasisi za Serikali na vyombo vyote vya ulinzi na usalama viadhimishe maadhimisho haya kwa kufanya shughuli za kijamii katika maeneo yao ya karibu au vikosi na kambi zao kama vile kufanya usafi, kupanda miti na kutoa huduma za afya.

"Kitendo hiki adhimu kitaleta hamasa kubwa, umoja na mshikamano na kuuenzi Muungano wetu kwa heshima na taadhima kubwa," alisema. Pia, alisema kutakuwa na maonesho ya Muungano yatayofanyika Zanzibar kuanzia Aprili 22, 2022 hadi Mei 6, ambayo yanahusisha Taasisi za Muungano.

# Uvuvi haramu sasa tishio Ziwa Victoria

**Na Richard Makore,**

MWANZA

JANGA la uvuvi haramu katika Ziwa Victoria limerudi kwa kasi na kutishia kutoweka kwa samaki kama hatua za haraka hazitachukuliwa kudhibiti hali hiyo.

Awali, serikali ilidhibiti uvuvi haramu katika ziwa hilo yakiwamo makokoro na kusaidia samaki aina mbalimbali wakiwamo sangara kuongezeka.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu janga hilo, Katibu wa Chama Cha Wavuvi Tanzania (TAFU), Jephat Machandalo aliiomba serikali kuongeza nguvu kudhibiti uvuvi haramu ambao alikiri umerudi kwa kasi.

Alisema kwa sasa samaki wadogo aina ya sangara wamezagaa mitaani katika mikoa yote ya Kanda ya Ziwa pamoja na maeneo mengine ambayo wanavuliwa kinyume cha sheria.

Katibu huyo ametaja aina tatu zinazotumika kufanikisha uvuvi huo ni pamoja na matumizi ya taa za sola kwa ajili ya kuvulia dagaa, makokoro pamoja na nyavu ndogo za dagaa kugeuzwa kuvulia sangara.

Alisema taa za sola ambazo zinatumiwa na wavuvi wa dagaa ambao ni wanachama wao pia, zinachangia kuibua samaki wadogo waliopo chini na kuja juu ya maji kutokana na mwanga wake kuwa mkali.

Aliongeza kuwa awali wavuvi hao walikuwa wakitumia taa za karabai ambazo hazina mwanga mkali ziwani na hivyo kufanya uvuvi uliozingatia taratibu na sheria.

"Hawa samaki wadogo wakipigwa na mwanga mkali wa sola wanapanda juu ya maji kutoka chini, hatua hii inasababisha samaki hawa kunaswa na nyavu za dagaa," alisema.

Machandaro alisema wavuvi wa dagaa wanatumia nyavu ndefu kwenda chini zaidi ya mita 20 na kusababisha kunasa samaki wadogo waliopanda juu na waliopo chini.

"Watu wanadhani nyavu za dagaa zinavua dagaa pekee, lakini haipo hivyo, hizi nyavu pia zinanasa samaki wadogo aina ya sangara na wengine ambao wanahitaji kukua na kuvuliwa wakiwa wakubwa," alisema Machandaro.

Kuhusu matumizi ya makokoro ambayo yamekatazwa kisheria, Machandalo alisema bado yapo na yanatumika katika maeneo mbalimbali huko ziwani na kw amba ameishatoa taarifa hiyo kwa serikali.

"Ni kweli kila soko katika maeneo ya Kahama, Simiyu, Tabora, Mwanza, Mara, Kagera, Geita hawa samaki wadogo utawakuta wakiuzwa, jambo ambalo ni hatari kwa kuwa siku chache zijazo kama hali hiyo haitadhibitiwa samaki wataisha ziwani," alisema.

Alibainisha kuwa kwa sasa wavuvi wa sangara wameamua kuhamia katika uvuvi wa kutumia nyavu za dagaa kwa kuwa wanatapata samaki wengi ingawa ni wadogo.

Aliongeza kuwa samaki hao wanavuliwa kwa wingi katika mialo mbalimbali na kusafirishwa kuanzia saa 10 hadi saa 12 asubuhi kwa kutumia pikipiki kuwapeleka sokoni.

Nyavu za kuvulia samaki kisheria zinatakiwa kuwa na matundu yenye ukubwa wa nchini sita na urefu wa kwenda chini kati ya mitaka 10 hadi 12.

Alitoa mfano kwa nchi ya Uganda ambayo imeweka masharti ya mtu anayetaka kuvua dagaa kwenda umbali wa mita zaidi ya 200 kutoka nchi kavu, lakini kwa Tanzania hakuna utaratibu wowote.

Alisema mvuvi anaweza kuvua sehemu yoyote zikiwamo sehemu za mazalia ya samaki ama kati kati ya ziwa kwenye kina kirefu bila kuulizwa na mtu.

Aliomba serikali kuweka mkazo katika suala hilo kwa kuwa isipofanya hivyo itarajie kumalizika kwa samaki siku chache zijazo.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe katika masoko mbalimbali, umebaini kwamba samaki wadogo aina ya sangara kwa sasa wanauzwa kwa mafungu.

Kwa sasa fungu moja lenye samaki sita hadi nane kutegemea na ukubwa linauzwa Sh. 2,000 na wafanyabiashara wakiwakaanga mmoja wanauza Sh. 2,000 hadi Sh. 3,000.

Akizungumzia sakata hilo, Ofisa Uvuvi Mfawidhi wa Kanda ya Ziwa, Roman Mkenda, alikiri kupokea malalamiko hayo.

Alisema kuna kundi la wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu ambao wanajihusisha na uvuvi haramu na kwamba wanaendelea kufanya doria ili kukomesha tatizo hilo.

Alikiri kuwapo upungufu kutoka kwa watendaji wakiwamo viongozi wa masoko, maofisa watendaji wa mitaa, vijiji na kata kwa kuwa samaki wanaovuliwa kwa njia haramu wanapitia huko.

Kuhusu matumizi ya taa za sola pamoja na nyavu za dagaa kutumika kuvulia sangara na samaki wengine, Mkenda alisema suala hilo wamelipokea kutoka kwa chama cha wavuvi na linafanyiwa kazi.

## Wanaopandisha bei vyakula waonywa

**Na Neema Hussein,** KATAVI

Mkuu wa mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, amewataka wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kupitia kamati za bei kuchukua hatua kali kwa wafanyabiashara wa mazao ya chakula wanaopandisha bei kiholela.

Mrindoko alitoa maelekezo hayo hayo katika kikao cha wadau wa kilimo kilichohusisha viongozi wa serikali, taasisi mbalimbali,wakulima, wafugaji na wafanyabiashara.

Alisema mazao yanayolimwa ndani ya mkoa huo hayatakiwi kupandishwa bei ili kuwafanya wananchi waweze kumudu kununua na kuendeleza ustawi wa mkoa huo.

Aidha Mrindoko alisema kitendo cha kupandisha bei ni kuhatarisha usalama wa mkoa huo na wao kama serikali hawatokubaliana na suala hilo.

"Swala lingine ni la wananchi kujiwekea akiba ya chakula pamoja na takwimu nzuri tulizonazo za mavuno tunayotarajia kuyavuna lakini tukirudi kwa mwananchi mmoja mmoja niwatake wananchi wote kuhakikisha wana akiba ya chakula ya kutosha angalau misimu miwili," alisema Mrindoko.

Alisema matarajio ya mavuno kwa msimu huu ni mazuri hivyo mkoa unatarajia kuvuna zaidi ya tani milioni moja na tayari baadhi ya mazao yameanza kuvunwa.

Mrindoko alisisitiza uzalishaji wa mazao ambayo yanatoa mafuta kwa kuwa msisitizo wa nchi kitaifa ni kulima kilimo cha alizeti ili kupunguza kiwango cha mafuta yanayotoka nje ya nchi.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara mkoa wa Katavi, Amani Mahela, alisema kama serikali haitaki bei kupanda basi inatakiwa mkulima apewe ruzuku kwa sababu mkulima analima mwenyewe, ananunua mbolea na vitu vingine, hivyo anatakiwa apewe uhuru wa kuuza.

"Serikali yetu inatakiwa kujua mkulima pia anatakiwa asomeshe watoto kwenye shule nzuri, anatakiwa aishi maisha mazuri na yeye atembelee gari hizo ni ndoto za wakulima na mimi tu niseme kwamba kiongozi mzuri ni yule anayeweza kuleta unafuu wa maisha kwa wale anaowaongoza lakini kuongoza watu masikini halafu unawawekea mipaka mi sioni kama ni sawa," alisema Mahela.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Hamad Mapengo, aliiomba serikali kuongeza maofisa ugani ili kufikia lengo walilokusudia na kuondokana na kilimo cha mazoea kama ilivyo kwa sasa.

# Utafiti wabainisha wanawake kutonufaishwa misitu ya asili

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

UTAFITI uliofanywa na Kituo cha Masomo ya Jinsia cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) umeonesha wanawake hawajanufaika katika kufikia na kutumia rasilimali zinazopatikana kwenye misitu ya asili.

Miongoni mwa rasilimali hizo ni uchomaji na biashara ya mkaa, mbao ni rasiliamali zinazopatikana kwenye misitu hiyo ikilinganishwa na wanaume.

Mkuu wa Kituo hicho, Prof. John Jeckoniah, alibainisha taarifa hizo mjini Morogoro alipowasilisha matokeo ya utafiti wake uliofanyika hivi karibuni uliokuwa unaangalia masuala ya jinsia na makundi maalumu katika utumiaji, ufikiaji na wanavyonufaika na rasilimali za misitu.

Prof. Jeckoniah alisema katika utafiti wao walitakiwa kuangalia mikakati gani inayotumiwa na wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwa ni pamoja na Mtandao wa Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) katika kubuni mikakati mbalimbali kuongeza ushiriki wa makundi maalumu hasa wanawake.

"Tumebaini kuwa kuna changamoto kadhaa za kukosekana kwa uwiano wa kijinsia kwenye makundi maalumu yanayoshiriki katika kutumia rasiliamali za misitu ya asili, na imeonekana wanawake hawanufaiki sana kama ilivyo kwa wanaume, " alisema Prof. Jeckoniah.

Alisema ,utafiti pia umebaini kazi kubwa imefanywa na mashirika hayo katika kuwajengea uwezo na kuboresha maisha na uchumi wa jamii kwenye vijiji mbalimbali vilivyofikiwa na miradi ya Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA).

Alisema mara nyingi suala la kijinsia huangalia zaidi wanawake na kusahau wanaume wakati nao wana mchango katika maamuzi na maoni kwenye familia.

Prof. Jeckoniah alisema utafiti huo umeonesha wanaume wakisahaulika kwenye mafunzo ya aina hiyo wakati wao ndiyo wanaotumika kutoa mawazo na maoni pamoja na usimamizi uko chini ya wanaume.

Naye Meneja Mradi wa Kuhifadhi Misitu kwa Kuwezesha Biashara Endelevu ya Mazao ya Misitu Tanzania (CoForEST), Charles Leonard, alisema lengo la tafiti hizo ni kuwashirikisha wadau na jamii kuhusu matokeo ya tafiti mbalimbali saba zinazohusu uhifadhi wa misitu zilizofanywa na watafiti kupitia mradi huo.

Alitoa wito kwa Serikali na wadau walio kwenye sekta ya misitu hususani misitu ya asili kutambua umuhimu wa misitu hiyo, na kwamba ipo haja ya kuangalia ni namna gani misitu hiyo iwe inasimamiwa vizuri.



Mbunge viti maalumu Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia Asasi za Kiraia, Neema Lugangira (wa tatu kulia), akiwa na Wabunge kutoka nchi ya Uswisi, walipokutana katika Ofisi za Ubalozi huo, jijini Dar es Salaam juzi. Wabunge hao, wapo hapa nchini kutembelea miradi inayofadhiliwa na nchi hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dola bilioni 1.2 zawekezwa kilimo kusini mwa Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) kimehamasisha wabia na wamewekeza Dola bilioni 1.2 katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania kuanzia mwaka 2010.

Lengo la kituo ni kuwekeza Dola bilioni 2.1 katika ushoroba huo ifikapo 2030.

Akizungumza katika mkutano wa wadau wa kilimo ambao ulijadili mada ya 'Mapinduzi ya Kilimo na Umuhimu wa kugawa vitendeakazi kwa maofisa ugani kilimo' uliofanyika hivi karibuni kwa njia ya mtandao, Mkurugenzi Mtendaji wa Sagcot, Geoffrey Kirenga, alisema katika uwekezaji huo sekta binafsi imeshiriki pakubwa na kuchochea uzalishaji wenye tija katika kilimo.

''Uwekezaji ulijielekeza katika kukuza uzalishaji, kuongeza thamani ya mazao ya chai, maziwa, uzalishaji wa vifaranga na chakula cha mifugo katika ushoroba wa Sagcot," alisema Kirenga Alisema lengo la Sagcot kati ya mwaka 2010 na 2030 ni kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza Dola bilioni 2.1 ili kuinua kilimo katika mikoa ya nyanda za juu kusini, kwani mikoa hiyo ni muhimu kibiashara kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

''Katika miaka 11 ya mwanzo (2010-2021) tayari sekta binafsi imewekeza Dola bilioni 1.2 na kuvuka lengo kwa 0.1 bilioni. Hizi ni jitihada kubwa katika kukuza na kuendeleza kilimo nchini," alisema Kirenga.

Alisema jitihada inayofanywa na Serikali katika kuboresha miundombinu imekuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha uwekezaji katika sekta za kilimo,mifugo na uvuvi.

"Jitihada hizi zitasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao nchini na kupunguza utegemezi wa kuagiza mazao ya chakula kutoka nje ya nchi kama ngano, sukari, mafuta ya kula na shayiri,"alisema.

Mafanikio mengine ambayo ameueleza mkutano huo katika kipindi hicho cha miaka 11 ni kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la viazi mviringo kutoka tani 7 kwa hekta 1 mpaka kufikia tani 28-50 katika hekta hivi sasa.

"Hii imetokana na matumizi ya mbegu mpya tisa za viazi na kufuata kanuni bora za kilimo jambo ambalo limeongeza uzalishaji na kusaidia kupunguza uagizaji wa viazi nje ya nchi ambapo nchi huagiza tani 30,000 za viazi mviringo kwa mwaka," alisema

Kirenga alieleza umuhimu wa kuweka katika mashamba makubwa ili kuinua uzalishaji wa kisasa na kushauri kwamba katika hali hiyo lazima wakulima wadogo watakaokuwa wamezunguka mashamba hayo washirikishwe, ili na wao waweze kukuza kilimo.

# Serikali kumwaga ajira 30,000 mwaka 2022/23

BUNGE limeelezwa katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imepanga kutoa kibali cha ajira kwa nafasi 30,000 zikiwamo nafasi za walimu.

Aidha, wahitimu 248,379 wa ualimu kwa ngazi mbalimbali wamehitimu kuanzia mwaka 2016 hadi Desemba, 2020.

Naibu Waziri wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Same Magharibi (CCM), Dk.David Mathayo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni lini Serikali itatoa vibali vya kuajiri walimu wa kutosha kukabiliana na ongezeko la wanafunzi na wahitimu wangapi wapo kwenye soko la ajira.

Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema idadi hiyo inajumuisha walimu wa Astashahada, Stashahada na Shahada na kati ya hao wameajiriwa na serikali na wengine sekta binafsi.

Aidha, alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali imetoa kibali cha nafasi 10,003 za ajira kwa walimu na kwa mwaka 2022/23 imepanga kutoa kibali cha ajira 30,000 ikiwamo za walimu.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Mbulu Mjini (CCM), Zacharia Issaay, alisema katika nafasi za kazi zaidi ya 30,000 zilizotangazwa na serikali lakini hakuna kada ya watendaji wa vijiji na kata na kuhoji lini serikali itatoa kibali cha kuajiri watendaji hao.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ndejembi alisema serikali ipo mbioni kuajiri watendaji wa vijiji na kata na watapangwa kwenye maeneo mbalimbali.

"Rai yangu kwa waajiri kuandaa orodha ya mahitaji yao kwenye watendaji wa vijiji, mitaa na kata na kuwasilisha TAMISEMI kwa wakati na kuileta utumishi ili zoezi la kuajiri litakapoanza tupeleke maeneo yote yenye uhitaji,"alisema.



Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa, akibadilishana mawazo na baadhi ya wabunge ndani ya ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bil. 70/- zatengwa kununulia vifaa tiba

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetenga Sh. bilioni 69.95 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwa zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri zilizokamilika.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Dk.Festo Dugange aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Josephine Genzabuke.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini Serikali itamaliza tatizo la ukosefu wa watumishi wa kada mbalimbali katika Hospitali pamoja na ukosefu wa vifaa tiba.

Akijibu swali hilo, Dk.Dugange alisema Serikali katika mwaka wa fedha 2020/21 iliajiri Watumishi wa kada za Afya 2,726 ambao walipelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Aidha, alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali inatarajia kuajiri watumishi 7,612 wa kada mbalimbali za afya ambao watapelekwa kwenye Halmashauri zote nchini.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Muhambwe (CCM), Dk. Florence Samizi, alitaka kujua mkakati wa serikali wa kujenga nyumba za watumishi.Naibu Waziri Dugange akijibu swali hilo, alikiri kuwepo na uhaba wa nyumba za watumishi na kwamba mpango wa serikali ni kuendelea kutenga fedha za mapato ya ndani na kutoka serikali kuu kuhakikisha nyumba za watumishi zinajengwa.

Mbunge wa Kishapu (CCM), Boniphace Butondo, alisema Wilaya ya Kishapu ina vituo vya afya vitatu ambavyo vimekamilika na kwamba vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi na kuhoji lini serikali itashughulikia tatizo hilo.

Dk.Dugange akijibu swali hilo, alisema vituo hivyo kweli vina upungufu wa watumishi na vifaa tiba na kwamba vituo hivyo vitapewa kipaumbele.

## Ahoji ujenzi barabara ya Tabora-Kangogwa

MBUNGE wa Bukene (CCM), Selemani Zedi, ametaka kujua sababu za kuchelewa kwa ujenzi wa barabara kutoka Tabora – Mambali – Bukene hadi Kangogwa ilhali ilishatengewa bajeti.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema kipande cha kilometa 65 katika barabara hiyo cha kutoka Nzega hadi Kagongwa ndicho kitatumika kubeba mzigo mkubwa wa mabomba ya mradi wa bomba la mafuta lakini hali ilivyo kwasasa barabara ni nyembamba na madaraja madogo.

"Nilishashauri Wizara ya Ujenzi ikae na Wizara ya Nishati pamoja na wanaotekeleza mradi ili kushughulikia barabara hiyo ipitishe mzigo huu mzito nauliza Wizara imefikia wapi kuhusu barabara hii ipitishe mzigo wa mabomba kwenda site,"alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alisema upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tabora – Mambali – Bukene hadi Kagongwa yenye urefu wa kilometa 114 umekamilika mwaka 2020.

"Baada ya kukamilika kwa Usanifu na gharama za ujenzi kwa kiwango cha lami kujulikana, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi,"alisema.

Aidha, alisema Serikali imejenga kilometa 9.6 kwa kiwango cha lami kutoka Tabora Mjini kuelekea Mambali.

"Mheshimiwa Spika, Wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kw kiwango cha lami, Wizara yangu kupitia TANROADS imeendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iendelee kupitika wakati wote,"alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 Sh. bilioni 1.2 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Hata hivyo, alisema wizara inaendelea kuratibu namna ya kushughulikia barabara itakayopitisha mabomba kwenda kwenye mradi wa bomba la mafuta.



ama
ALHAMISI APRILI 21, 2022
AFYA NA MAZINGIRA


Ukurasa 12

Daktari bingwa: Hivi hapa visababishi vikuu vya saratani, maisha kukatizwa


Ukurasa 13

Wanamazingira NEMC, wasomi SUA waingia ubia mradi kukabili tabianchi



Ukurasa 14

Mkurugenzi TACAIDS: Tumefanikiwa kuupunguza Ukimwi hapa nchini

AFYA

## UBIA KITUO CHA SERIKALI & AGA KHAN

# Waziri Ummy atoa neno mbinu za umma kukabili janga saratani

**Na Yasmine Protace**

SARATANI ni ugonjwa unaotajwa kuchangia vifo kwa wengi na kusababisha kifo, hasa pale mgonjwa anapochelewa kupata matibabu kwa wakati. Ni ugonjwa unaojitokeza kwa namna mbalimbali, hivyo muhimu ni kuwahi kupata matibabu yake.

Mtu anapofanikiwa kuchunguza afya yake na akagundua kinachosumbua, inakuwa rahisi kwake kupata matibabu na kinyume chake kwa wanaochelewa kuanza tiba au uchunguzi.

Baadhi ya watu wanaochelewa, hujigundua wako kwenye matatizo ya kiafya ya kuchelewa wakiwa wamechelewa kuanza matibabu.

Inatajwa kama mtu atakuwa amegundulika mapema kuwa na ugonjwa wa saratani atapatiwa matibabu na ataendelea na maisha yake.

Wapo waliogundulika mapema kuwa wanasumbuliwa na ugonjwa huo, pamoja na kugundulika wamekuwa wakipatiwa matibabu na kuendelea na majukumu yao ya kila siku.

Kwa wale ambao wanachelewa kupata matibabu kutokana na kugundulika wakiwa wamefikia hatua za mwisho, mara nyingi watu hao huwa wanapoteza maisha.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu anakumbusha kwamba, serikali imekuwa ikitanganza kwa kuwataka wananchi wajitokeze kuchunguza afya zao, lengo ni kuwasaidia watakaogundulika kuwa na tatizo, waweze kupatiwa matibabu mapema iwezekanavyo.


Waziri wa Afya, akishiriki uzinduzi wa Kituo cha Saratani kinachoendeshwa kwa ushirikiano na serikali, hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

Kimsingi, panapotokea uchunguzi wa magonjwa unafanywa, anaeleza ni wajibu wa jamii kujitokeza ili kuweza kuchunguzwa na itakapobainika anasumbuliwa na ugonjwa wowote, inakuwa rahisi kupatiwa matibabu.

Waziri anakumbusha kwamba, utaratibu uliopo ni pale mtu anapogundulika mapema anaumwa, inakuwa rahisi kwake kupatiwa matibabu.

Hivi karibuni serikali imeainisha kwamba, kuchelewa kugundua maradhi ya saratani imetajwa kuwa sababu kubwa inayochangia vifo kwa saratani kwa kuwa inakuwa ngumu kutibika.

Waziri Ummy akizungumza kwenye tukio la uwekaji wa jiwe la msingi kwenye ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Matibabu ya Saratani ambacho kinatekelezwa kwa ubia kati ya serikali pamoja na taasisi ya Agha Khan, jijini Dar es Salaam.

Waziri Ummy anasema, Tanzania inakadiriwa kuwa na wagonjwa wapya wa saratani 42,060 kila mwaka ikiwa ni sawa na wagonjwa 76 katika kila watu 100,000 huku vifo vikiwa ni 29,000 kila mwaka sawa na asilimia 68.

Waziri Ummy amesema, wagonjwa wengi wa saratani wanagundulika ugonjwa ukiwa umefika katika hatua ya tatu au ya nne, ambayo ni ngumu kutibika, akitaja sababu ya kuchelewa kugundua saratani ni pamoja na kuwa na vituo vichache vinavyotoa huduma hiyo nchini.

"Kutokana na changamoto ya vituo vichache vya kupima na kutoa matibabu ya saratani nchini, serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeingia ubia na Agha Khan (Foundation) kutekeleza mradi huu ambao utatusaidia kuwafikia watanzania wengi kupata huduma za kupima pamoja na kupata matibabu ya saratani,"anasema.

Waziri Ummy anaongeza kuwa, kituo hicho kinatarajia kuhudumia wagonjwa wa saratani takribani 120 kwa siku, hivyo itaweza kuipunguzia mzigo taasisi ya saratani ya Ocean Road, ambayo inahudumia wagonjwa 800 mpaka 900 kwa siku.

Aidha, Waziri Ummy amewataka Watanzania kujitokeza mapema na kuwa na utamaduni wa kufanya uchunguzi wa afya zao mara kwa mara ikiwemo saratani.

Waziri Ummy anataja saratani ambazo zinaongoza nchini, ni pamoja na saratani ya mlango wa kizazi wanawake, saratani ya matiti pamoja na saratani ya tezi dume huku maeneo ambayo yanaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi ni mikoa ya Kanda ya Mashariki (61%), Kanda ya Kaskazini (17.3%) na Kanda ya Ziwa (9.1%).

AFYA

# Daktari bingwa: Hivi hapa visababishi vikuu vya saratani, maisha kukatizwa

## • Tezi dume, shingo kizazi zinavyotua mwilini



Mkurugenzi wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage akitoa maelezo kwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuhusu ufanisi wa mashine ya mionzi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

KATIKA jamii kuna saratani ya tezi dume, ambayo ni shida ya maradhi inayotajwa kuwapo kwenye seli zilizoko kwenye tezi dume kwa wanaume, huku saratani ya shingo ya kizazi ikiongezeka zaidi kwa kinamama.

Mwaka 2020, takwimu za maambukizi mapya zilikuwa 10,241 huku kila mwaka wanawake 9,772 hugundulika kuwa na ugonjwa huo.

Pia, mwaka 2018 saratani ya tezi dume ilikuwa asilimia 7.1 ya saratani zote zilizowapata watu na ilisababisha asilimia 3.8 ya vifo vyote vya saratani, duniani.

**MAONI YA BINGWA**

Bingwa wa Magonjwa ya Saratani kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Caroline Swai, anasema vihatarishi vya saratani ya tezi dume, dalili na ugunduzi ikifuatiwa na matibabu, ni hatua ambazo baadhi hushindwa kuzitambua mapema.

Anasema, saratani tishio ni ya shingo ya kizazi, matiti na tezi dume na zimetajwa kuwa kati ya aina takribani 10 za ugonjwa huo, zinazoongoza kwa ongezeko la wagonjwa na vifo nchini, huku wanawake wakiathiriwa zaidi.

Dk. Caroline amebainisha hayo mkoani Dar es Salaam, alipowasilisha mada kuhusu aina tatu kuu za ugonjwa huo, kwenye mafunzo ya kuwajengea uelewa wanahabari katika mafunzo yalitolewa na Mradi Mtambuka wa Saratani (TCCP).

Ni mradi huo uliofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) na asasi ya Aga Khan Foundation (AKF) unatekelezwa kwa miaka minne na mtaalamu

> **Kuchelewa kupata mtoto wa kwanza baada ya umri wa zaidi ya miaka 30, kutowahi kabisa kubeba mimba na kutonyonyesha, kutokufanya mazoezi na unene uliokithiri (obesity) ni sababu mojawapo.**

anasema, mtu mwenye saratani ya tezi dume anakuwa na dalili kadhaa.

Anaitaja kuwa ni kujisikia kukojoa mara kwa mara na wakati mwingine kwa dharura, kupata shida katika kuanza au kuzuia mkojo, maumivu wakati wa kukojoa na kujamiiana.

"Mtu mwenye saratani ya tezi dume huweza pia kupata dalili hizi... damu kwenye mkojo au manii, maumivu kwenye kiuno, nyonga na mgongo," anasema Dk. Caroline.

**SABABU NINI?**

Bingwa huyo anasema visababishi vya tezi dume, pia vinaongeza uwezekano wa mtu kupata saratani aina hiyo, akitaja kigezo kimojawapo, yaani kuwa na umri zaidi ya miaka 50.

Pia, anafafanua ndugu aliyewahi kupata saratani ya tezi dume, anaweza kurithiwa kupitia vinasaba vyenye hitilafu kutoka kwa wazazi, akidokeza mara nyingi utafiti ulishabaini watu wenye ngozi nyeusi au wenye asili ya Kiafrika wako hatarini zaidi, ikilinganishwa na jamii tofauti.

"Ulaji nyama nyekundu na mafuta ya wanyama huongeza hatari, uvutaji sigara na unywaji pombe kupita kiasi, navyo ni visababishi vya saratani," anaeleza Dk. Caroline.

**VIPIMO VINAVYOTUMIKA**

Dk. Caroline anasema kwa upimaji saratani hiyo, baadhi ya watu wanahofia, kutokana na mbinu iliyokuwapo awali ya kutumia kidole, ila sasa kuna vipimo kadhaa vinatumika, ikiwamo damu kuchunguzwa protini maalum ya tezidume (PSA) na kipimo cha kuchunguza ukubwa na umbo hufanyika kama vipimo vya awali.



Bingwa wa Magonjwa ya Saratani kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Caroline Swai.

"Kipimo cha maabara cha kuchunguza kinyama kutoka kwenye tezi dume hufanyika kuhakiki saratani ya tezi dume. Vipimo vya picha (kama mammography, X-ray, ultrasound, CT scan, MRI na PET scan) huweza kufanyika kuchunguza dalili na hatua ya saratani ilipofikia," anafafanua.

Dk. Caroline anasema hakuna kinga ya kumzuia inayomuwezesha mtu asipate kabisa saratani ya tezi dume, ingawa ipo nafasi kupunguza uwezekano wake kupitia kubadili tabia hatarishi, ikiwamo matumizi ya tumbaku na pombe iliyokithiri, kwa mbadala kuegemea ulaji matunda na mboga za majani.

Anafafanua kuwa, kupunguza ulaji wa vyakula vya mafuta, chumvi, mafuta ya wanyama, nyama nyekundu, vyakula vilivyosindikwa, vinachangia kupunguza au kuondoa uwezekano wa kuugua ugonjwa huo.

Mtaalamu huyo anataja kinga rahisi na isiyo ghali ni kwa mtu kufanya mazoezi angalau mara mbili mpaka tatu kwa wiki, iwe kutembea au kufanya shughuli yeyote kwa nusu saa, ili kuruhusu damu kuzunguka vyema.

**SARATANI MATITI**

Bingwa huyo anasema, saratani huanzia kwenye seli zilizoko kwenye matiti na inawapata watu wa jinsia zote, wengi wakiwa kinamama na kinababa ni asilimia moja.

Mtaalamu huyo anasema, takwimu za mwaka 2018 zinaonyesha saratani ya matiti ilikuwa asilimia 11.6 ya saratani zote zilizowapata watu na ilisababisha asilimia 6.6 ya vifo vyote vya saratani duniani.

Takwimu za 2020 zinaonyesha kulikuwapo na maambukizi 3,992, kati yao kuna wanaume asilimia moja .

**DALILI ZAKE ZILIVYO**

Dk. Caroline anasema ugonjwa ukiwa kwenye hatua za awali mtu anaweza asiwe na dalili zozote au maumivu kwenye titi na eneo kuzunguka titi.

Anasema dalili zinazoweza kujitokeza ni uvimbe mdogo au mkubwa kwenye matiti, kubadilika umbo, ukubwa na mwonekano, kuvimba, kuwasha, kubadilika ngozi ya titi na kuwa na madoa au vishimo kama ganda la chungwa au hata kutokwa na maji au damu kwenye chuchu.

"Kuchubuka kuzunguka chuchu, au chuchu kuingia ndani vilevile chuchu kupata kidonda ni dalili" anafafanua mtaalamu Dk. Caroline.

**SABABU ZILIZOKO**

Bingwa huyo anasema uwezekano kupata saratani ya matiti ni jinsi, akisema wanawake wako hatarini zaidi kuliko wanaume.

Pia, anautaja umri kuwa sababu ya pili kwa wenye zaidi ya miaka 50, hali kadhalika historia binafsi ya kuwahi kuugua saratani hiyo.

Sababu zingine, ni kuanza kupata hedhi mapema chini ya umri wa miaka 12 na kuchelewa kukoma hedhi baada ya miaka 55.

"Kuchelewa kupata mtoto wa kwanza baada ya umri wa zaidi ya miaka 30, kutowahi kabisa kubeba mimba na kutonyonyesha, kutokufanya mazoezi na unene uliokithiri (obesity) ni sababu mojawapo," anabainisha bingwa huyo.

"Mwanamke ambaye amekoma hedhi, anachagua siku yoyote katika mwezi ya kujifanyia uchunguzi. Mwanamke huweza kujichunguza mwenyewe akiwa anaoga au amekwishaoga kwa kusimama mbele ya kioo au akiwa amelala.

"Aweke mikono chini, juu, au kiunoni na kuangalia rangi, ukubwa wa matiti na kulinganisha la kushoto na lile la kulia. Kiganja cha kushoto kitapima titi la kulia na kiganja cha kulia kitapima la kushoto kwa kuzunguka ziwa lote.

INAENDELEA UK.13

MAZINGIRA

# Wanamazingira NEMC, wasomi SUA waingia ubia mradi kukabili tabianchi

Na Joseph Mwendapole

MABADILIKO ya tabianchi, kimsingi yanafafanuliwa kuwa ongezeko la muda mrefu la joto la wastani duniani linalosababisha kubadilika mfumo mzima wa hali ya hewa, ambao mara nyingi huleta athari hasi kwenye uso wa dunia.

Hizo ni kama vile ukame, mafuriko, kuongezeka joto, kuvurugika mifumo ya ikolojia katika majira ya mwaka, kuongezeka kina cha bahari, kusambaa magonjwa na hata kutokea kwa vimbunga.

Mabadiliko ya tabianchi yanatajwa kuwa ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazoikabili jamii yetu na Dunia kwa ujumla katika zama hizi.

Shughuli za kibinadamu za kujitafutia maendeleo kama vile ongezeko la shughuli za viwanda duniani hasa vinavyotumia nishati ya masalia ya viumbe hai.

Nishati hizo ni kama vile mafuta na makaa ya mawe, ukuaji sekta ya usafirishaji, uzalishaji nishati ya umeme kwa vyanzo vinavyozalisha gesijoto, kukatwa misitu kwa njia zisizo endelevu ni baadhi tu ya shughuli zinazozalisha gesi joto na kuongeza tatizo la mabadiliko ya tabianchi.

Serikali ya Tanzania ilisha ridhia mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabianchi ambao nchi wanachama zilianzisha mifuko mbalimbali ya kushughulikia changamoto hizo za mabadiliko ya tabianchi.

Mfano mmojawapo, unajulikana kwa jina'Adaptation Fund (AF)' unaowezesha nchi wanachama zinazoendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kinachoitwa 'Green Climate Fund' ambayo inasaidia kuzuia ongezeko la joto duniani na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kupitia fursa hiyo, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), lilipata ithibati ya kuwa na mfuko 'Adaptation Fund' na kuiwezesha Tanzania kupatia fedha za kutekeleza miradi mbalimbali kwa bara na visiwani, kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.



Mratibu wa Huduma za Macho Wilaya ya Kibaha, Sarah Mghwira, akimfanyia uchunguzi wa macho mtoto wa darasa la awali. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON**

### KULIKOPIGA HATUA

Miongoni mwa miradi inayotekelezwa, inahusu uvunaji maji wa kimkakati, hata kuwezesha kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa wakazi wa vijijini katika nyanda kame nchini (SWAHAT), unaotekelezwa katika mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora.

Mradi wa SWAHAT unatekelezwa na Chuo Kikuu Cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na unasimamiwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Ni mradi unaotarajiwa kumalizika ndani ya miaka minne, pia utanufaisha wilaya nne katika mikoa iliyopendekezwa, ambayo ni Bahi (Dodoma), Manyoni (Singida), Igunga (Nzega) mkoani Tabora.

Mradi wa SWAHAT unalenga kutekeleza mambo yafuatayo ili kuwezesha wanufaika kuhimili mabadiliko ya tabianchi, pia kuna kujengwa na kukarabatiwa mabwawa ya kuvuna maji, ili kuwezesha shughuli za kilimo, mifugo na kuchimba visima vya maji kwa matumizi ya binadamu.

Mtazamo uliopo, ni kwamba kuandaa kutekeleza mpango shirikishi wa upandaji miti ya matunda, kuni na mbao na katika kutekeleza shughuli hizo, wananchi wa maeneo husika watajipatia vyanzo madhubuti vya maji, kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Inaelezwa, miundombinu ya umwagiliaji kuwezesha kilimo cha mboga itajengwa, visima vya maji vitachimbwa kwa ajili ya matumizi nyumbani, pamoja na kujengwa malambo ya kunywesha mifugo.

> **Mfuko wa Adaptation Fund (AF), ni mojawapo ya fursa za wazi kwa nchi kutatua baadhi ya changamoto za mabadiliko ya tabianchi.**

Aidha, mradi wa SWAHAT unatarajiwa kuwezesha shughuli za kujiongeza kipato katika njia inayozingatia uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kama vile uanzishaji vitalu vya miti, upandaji miti kwa matumizi uhifadhi wa mazingira na kufuga samaki.

Vilevile wataalamu hao kutoka SUA, wana matarajio kwamba wataandaa na kuwezesha utekelezaji mbinu za kukabiliana na wadudu waharibifu na magonjwa ya mifugo, pia mimea inayojitokeza kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi, ili kuboresha uzalishaji wa kilimo na mifugo.

Mfuko wa Adaptation Fund (AF), ni mojawapo ya fursa za wazi kwa nchi kutatua baadhi ya changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, kuna fursa nyinginezo ambazo jamii inaweza kuzitumia kuleta maendeleo na uhimili wa mabadiliko ya tabianchi. Ni fursa zinazotegemea uwepo wa mifumo thabiti katika kutekeleza miradi kwa uhakika na kwa wakati, ili kuepuka madhara hasi yaletwayo na mabadiliko ya tabianchi.

### JICHO KWA WANUFAIKA

Wanufaika wa mradi huo wa SWAHAT, wanaelekezwa kuhakikisha athari zote zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi zilizolengwa kutatuliwa na mradi huo, zinapungua.

Pia, inatajwa wananchi waongeze kipato kupitia uzalishaji mazao kwa njia ya umwagiliaji, hasa pale mabwawa yatakapojengewa na karabatiwaa. Lingine linatajwa ni kuboreshewa shughuli za kilimo, mifugo, ufugaji samaki na kuwezesha mfumo mzuri wa upandaji miti kwa ajili ya matunda, kuni, mbao na vitalu vya miti.

Halmashauri husika nazo zinaaswa kufuatilia shughuli za mradi, kujifunza, kuendeleza, kuiga na kuzipeleka katika maeneo mengine kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato vikiwemo vya ndani ili kufanya matokeo ya mradi yawe endelevu.

## Daktari bingwa: Hivi hapa visababishi vikuu vya saratani

INATOKA UK.12

"Kisha atapima kwenye chuchu na kukamua kuona kama linatoa majimaji au damu, kisha ataangalia kama tezi za kwapani zimevimba," anaeleza.

### HALI IKOJE

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema Tanzania inakadiriwa kuwa na wagonjwa wapya wa saratani 42,060 kila mwaka ikiwa sawa na wagonjwa 76 katika kila kundi la watu 100,000, huku vifo navyo vinagota kwa watu 29,000 kila mwaka sawa na asilimia 68.

Anataja sababu kuu ni kuchelewa kugundua saratani hata kuchangia iwe ngumu kutibika na Ummy anabainisha hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam alipoweka jiwe la msingi la ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha matibabu ya Saratani, kinachotekelezwa kwa ubia kati ya serikali na taasisi ya Agha Khan.

"Wagonjwa wengi wa saratani wanagundulika ugonjwa ukiwa umefika katika hatua ya tatu au ya nne, ambayo ni ngumu kutibika," anasema kwa kufafanua, sababu ya kuchelewa kugundua saratani, ni pamoja na kuwapo vituo vichache vya kutoa huduma hiyo nchini.

"Kutokana na changamoto ya vituo vichache vya kupima na kutoa matibabu ya saratani nchini, serikali imeingia ubia na Agha Khan kutekeleza mradi huu ambao utatusaidia kuwafikia Watanzania wengi kupata huduma za kupima pamoja na kupata matibabu ya saratani," amesema Ummy.

Waziri anasema, ni kituo kinachotarajiwa kuhudumia wagonjwa wa saratani takribani 120 na kupungua mzigo kwa sasai ya kansa Ocean Road, inayohudumia wagonjwa 800 mpaka 900 kwa siku.

Waziri anataja saratani zinazoongoza nchini ni: Mlango wa kizazi kwa wanawake; matiti; na ya tezi dume. Pia, maeneo yanaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi, yanatajwa kuwa ni mikoa ya kanda ya Mashariki kwa asilimia 61, kanda Kaskazini (17.3%) na Kanda ya Ziwa (9.1%).

AFYA

# Mkurugenzi TACAIDS: Tumefanikiwa sana kuupunguza Ukimwi hapa nchini

- Waumiza vichwa kunusuru mabinti na hatma zao
- Wasema lengo la tija kimataifa limefikiwa nchini



kurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, akitoa elimu ya kinga dhidi ya VVU kwa walimu (hawako pichani). **PICHA: NADHIFA OMAR wa TACAIDS**

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KWA kurejea utafiti wa viashiria vya virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi wa mwaka 2016/2017, kundi la vijana wa miaka 15 hadi 24 ndilo lililoathiriwa zaidi na maambukizi mapya ya VVU.

Hali kadhalika, nchini Tanzania ina jumla ya watu 1,700,000 wanaoishi na VVU na tayari wanatumia dawa za kuvifubaza (ARV).

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kuthibiti UKIMWI nchini (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, anasema takwimu zinaonyesha maambukizi mapya ya VVU kwa mwaka ni watu 68,000.

Anaendelea kufafanua: "Pamoja na kuonekana kupungua kwa maambukizi, bado kundi la vijana lipo kwenye hatari zaidi, hasa wasichana. Takribani asilimia 30 hadi asilimia 40 ya vijana wanaopata maambukizi mapya ya VVU, asilimia 80 ni vijana wa kike," anaeleza.

Ili kulinusuru kundi hilo la vijana ambalo ndilo tegemeo katika jamii na nguvu kazi ya taifa, TACAIDS imekuja na mpango wa kutoa elimu ya VVU na Ukimwi, afya ya uzazi na stadi za maisha kwa walimu wa shule za msingi na sekondari, kwa kuzingatia watoto na vijana balehe wanatumia muda mrefu shuleni.

Anasema kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu, Ukimwi na Malaria (GFATM), TACAIDS inaratibu Mradi 'Timiza Malengo' ambao

> **"Walimu watasaidia pia katika suala la uundaji wa klabu za kudhibiti Ukimwi na afya kwa wanafunzi, ambapo mojawapo ya ajenda itakuwa ni kuzuia na kudhibiti maambukizi mapya ya VVU.**

kuna shule 1,961 na walimu 3,923 katika halmashauri 18 za mikoa ya Tanga, Morogoro, Singida na Dodoma wameshafikiwa.

"Elimu hiyo inahusisha pia VVU na Ukimwi, afya ya uzazi, stadi za maisha na Uviko - 19, ili kuwaongezea ujuzi walimu katika maeneno ya shule na kuwawezesha kusambaza maarifa ndani na nje ya taasisi.

"Tafiti zinasema maambukizi ni makubwa kwa vijana wa kike kutokana na kuanza ngono katika umri mdogo wa miaka 10 bila kinga," anaeleza Dk. Maboko, akitaja kundi la walimu ni muhimu, kwani lina uwezo kufikisha elimu hiyo haraka na kwa wakati mmoja, nchi nzima.

Anakiri tume haina uwezo kutekeleza pasipo kushirikiana na wadau kama walimu, ambao ni sehemu ya wazazi ambao muda mrefu wako karibu na wanafunzi, hali inayorahisha mawasiliano ya utoaji elimu ya VVU na Ukimwi, afya ya uzazi, pia stadi za maisha.

"Walimu watasaidia pia katika suala la uundaji wa klabu za kudhibiti Ukimwi na afya kwa wanafunzi, ambapo mojawapo ya ajenda itakuwa ni kuzuia na kudhibiti maambukizi mapya ya VVU," anasema.

Pia, wanafunzi nao watasaidia kufikisha elimu husika kwa wanajamii wengine, ili mwitikio wa UKIMWI uzidi kuwa endelevu na mtambuka.

"TACAIDS inalenga pia kuwashirikisha maofisa na wadhibiti ubora na wakaguzi wa elimu, ili wasaidie kutilia mkazo na kusimamia utoaji wa elimu ya VVU kwa wanafunzi.

"Hatua hiyo itasaidia pia kuzuia mimba za utotoni, ukatili wa kijinsia, matumizi ya dawa za kulevya, tumbaku na pombe ili watoto waweze kumaliza salama elimu zao na kutimiza malengo yao ya maisha watakayokuwa wamejiwekea,"anasema.

Kwa mujibu wa Dk. Maboko, vijana walio nje ya mfumo rasmi wa masomo watapata elimu ya kujikinga na VVU, biashara, kuandaa andiko la biashara, kulingana na matakwa ya kila mlengwa.

Pia, anawataja wasichana balehe na wanawake vijana hao watapatiwa mtaji wa kuanzisha shughuli zitakazowawezesha kiuchumi. Anasema tafiti zinaonyesha kwamba, kundi hilo ni miongoni mwa vijana walio katika mazingira hatarishi kuambukizwa VVU, kwani baadhi wamekuwa wakijiingiza kwenye ngono isiyo salama, kukidhi mahitaji yao na familia.

### MAFANIKIO LUKUKI

Hadi sasa TACAIDS inajivunia mafaniko iliyoyafikia, ikiwamo kupungua kwa vifo vitokanavyo na UKIMWI kwa asilima 50, kutoka 64,000 mwaka 2010 hadi 32,000 mwaka jana, akitafsiri ni mwitikio bora wa wadau wakiwemo Wizara ya Afya na wadau.

Aidha, kwa watu wazima kiwango cha maambukizi mapya ya VVU kinatajwa kupungua kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka jana.

Hali kadhalika, takwimu zinataja maambukizi mapya ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, yameshuka kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia saba, mwaka 2021.

"Aliendelea kueleza kuwa matumizi ARVs kwa wenye maambukizi ya VVU yameongezeka kutoka asilimia 95 mwaka 2016 hadi asilimia 98 mwaka jana," anasema Dkt Maboko.

Kwa mujibu wa TACAIDS, serikali hadi sasa inatekeleza vyema shabaha za kimataifa za tiba, Tanzania ipo kwenye hatua nzuri za kufikia malengo ya kidunia ifikapo mwaka 2025.

Anafafanua, kwamba ni asilimia 95 ya wanaojua hali zao wawe wameshaanza kutumia dawa za kufubaza VVU (ARV); na asilimia 95 ya wale wanaotumia ARV wawe wamefubaza VVU katika miili yao.

Hadi sasa watu wenye maambukizi ya VVU (WAVIU) wanaofahamu hali zao za mambukizi ni asilimia 83, waliopo kwenye matibabu asilimia 98 na waliofubaza VVU wako asilimia 92.

### UNYANYAPAA WASHUKA

Hali ya unyanyapaa na ubaguzi kwa mujibu wa takwimu za kitaifa, kiwango kimepungua kutoka asilimia 28 mwaka 2013 hadi asilimia 5.5 mwaka jana.

Kwa maendeleo endelevu ya kudhibiti VVU, hivi sasa TACAIDS inafanya mapitio ya Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi, hata imefanikiwa kukamilisha miongozo mingine muhimu. Anaorodhesha kuwa ni:

Mkakati wa Taifa wa Uwekezaji kwenye Ukimwi wa mwaka 2020; Mwongozo wa Kitaifa wa Sekta Zote wa Utekelezaji Afua za Kudhibiti Unyanyapaa na Ubaguzi unaohusiana na VVU na Ukimwi (Faharisi ya UKIMWI).

Mingine ni: Mwongozo wa Kuwawezesha Watendaji Muhimu kufanya Afua za Ukimwi kwenye bandari, maziwa na jamii inayozunguka maeneo hayo wa mwaka 2020; na Mwongozo wa Utoaji wa huduma za kudhibiti VVU na UKIMWI katika maeneo hatarishi na mpakani, pia Mkakati wa Mawasiliano, Mkakati wa Taifa wa Kondomu na Mkakati wa Uratibu wa Asasi za Kiraia.

Anasema, tume hiyo imeweza kutoa elimu ya sheria ya VVU na Ukimwi na haki za binadamu iliyowahusisha wadau mbalimbali, katika kujua haki na wajibu wa watu wanaoishi na VVU, masuala ya unyanyapaa, ubaguzi wake, pia ukatili kijinsia.

Makundi ya wadau waliofikiwa na elimu hiyo yanajumuisha wavuvi, vijana, Polisi- Dawati la Jinsia, mahakimu, waendesha mashtaka, waratibu wa mikoa na halmshauri, jeshi la magereza, maofisa ustawi wa jamii, na waajiri.





## Ujio makao makuu wabadilisha maisha

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, amesema ujio wa makao makuu Dodoma umebadilisha maisha ya wakazi wa Dodoma pamoja na kuleta mabadiliko ya nyumba za ibada.

Aidha, amesema Tanzania ni nchi pekee ambayo mikusanyiko ya kidini haibagui mtu yeyote.

Mavunde alisema hayo jana katika hafla ya futari ya mfungo wa Mwezi mtukufu wa Ramadhani iliyoandaliwa na Taasisi ya The Dodoma General Muslim Association (DGMA) jijini hapa.

Alisema ujio wa makao makuu umeongeza waumini wa dini mbalimbali na kusababisha kupanua majengo ya nyumba za ibada ili kupokea idadi kubwa na ujenzi wa nyumba hizo kujengwa ili kuendana na hadhi ya makao makuu.

"Kwa sasa makao makuu Dodoma ukipita kwenye nyumba za ibada zimejengwa vizuri kutokana na viongozi wakuu wa nchi na kidini kuhudhuria maeneo hayo wakati wa ibada,"alisema.

Aidha alisema misingi ya umoja iliyojengwa na serikali imekuwa ikiwakusanya jamii bila ubaguzi wa dini.

"Najua futari ni kwa ajili ya wenzetu mliofunga lakini kutokana na upendo na umoja wetu mmealika hata ambao sio wa imani yenu huu ndio umoja tulio nao Tanzania," alisema.

Kadhalika alisema kutokana na umoja huo kila kundi la imani nyingine limekuwa likishirikiana na wengine bila ubaguzi.

Alibainisha kuwa mikusanyiko ya kijamii au kidini imekuwa ikijenga umoja na ushirikiano katika jamii yetu bila kujali kabila wala dini ya mtu.

Aliongeza kuwa ofisi yake itaendelea kushirikiana na makundi yote na ipo tayari kushirikiana na waumini wa dini ya Kiislamu kujenga uzio wa uwanja wa makaburi eneo la Kizota jijini hapa.

Pia alisema wataendelea kushirikiana na wananchi wa dini mbalimbali katika ujenzi wa nyumba za ibada.

Mlezi wa Taasisi hiyo, Ismail Dawood, alisema wamekuwa na utaratibu huo wa kufuturisha kila mwaka ikiwa ni sehemu ya kushirikiana na makundi ya watu wote.

Dawood alisema wamekuwa na utaribu wa kuwaalika viongozi wa serikali na viongozi wa dini ya Kikristo katika futari hiyo ili kuonyesha umoja wa makundi yote.

Katibu wa DGMA, Twalibu Twalibu alisema lengo kuu la Taasisi hiyo ni kuleta ustawi kwa waislamu Mkoa wa Dodoma.

Twalibu alisema taasisi hiyo ilisajiliwa mwaka 1954 na ilisaidia katika harakati za kuleta uhuru wa Tanzania kutokana na kushirikiana na viongozi wa dini na serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri, aliwataka wananchi kuchangamkia fursa za uchumi na ajira za kazi ya ujenzi kwenye eneo la mji wa serikali Mtumba Jijini hapa.

Alisema kuna ujenzi wa majengo makubwa ya wizara mbalimbali hivyo wananchi wajitokeze kuchangamkia fursa hizo za kiuchumi zilizoletwa na serikali.

# Jiji latoa msimamo machinga kuhamishwa soko la Sabasaba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya wafanyabiashara wa soko la Sabasaba jijini Dodoma kutishia kuandamana kwenda bungeni kumwona Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ili kumfikishia kilio chao cha kuondolewa bila kushirikishwa, Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, amejitokeza kutolea ufafanuzi sakata hilo.

Mafuru akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, alisema lengo la serikali ni jema kwa maslahi ya wafanyabaishara hao na si vinginevyo.

Alisema lengo la jiji ni kuwahamisha kwa muda ili kufanya ukarabati wa soko hilo na baadaye watawarejesha kuendelea na shughuli zao kama ilivyo sasa.

"Soko hili limekuwa la muda sana toka mwaka 1996 halijafanyiwa ukarabati. Miundominu yake ni mibovu sana ndiyo maana leo hii mvua ikinyesha tope linakuwa la kutisha na tunapokea simu za malalamiko kuwa tunachukua ushuru lakini hatufanyi ukarabati," alisema Mafuru

Mafuru alisema jiji halina lengo la kuwaonea wafanyabiasahara bali kinachotakiwa ni kuwashirikisha kila hatua ili kupata uelewa wa pamoja na kila mtu kuridhika na uamuzi huo.

"Lengo ni kufanya uhakiki kwanza kutambua nani anamiliki nini na anafanya nini. Kuna watu wana hofu kuwa tunakwenda kuwaondoa. Tunachokwenda kufanya ni kuwahamisha kwa muda ili kupisha ujenzi wa eneo hilo kwa muda wa mwaka mmoja au miwili kulingana na mchoro wetu," alisema Mafuru.

Pia alisema malalamiko ambayo wamekuwa wakiyapata yanaonyesha kuwa wafanyabiashara hao hawana imani na jiji katika kutekeleza mpango huo.

Alisema ili kupata kauli moja wanapanga kuendelea na vikao vya kujadilina baina ya jiji na uongozi wa soko hilo ili kupata namna bora ya kufikia mwafaka.

"Kuna watu wana hofu kupoteza vibanda vyao hasa wale wenye maeneo zaidi ya moja. Lakini niwahakikishie kuwa kupitia mazungumzo tutafikia mwafaka, hakuna atakayepoteza haki yake. Waelewe tu tunafanya uhakiki ili kujiridhisha na idadi ya wafanyabiashara iliyopo," alisema.

Mkuu wa Idara ya Fedha Jiji la Dodoma, Rahabu Philip, alikanusha taarifa kuwa wafanyabiashara hao hawajashirikishwa katika mpango huo wa jiji.

"Tumekuwa tukiwashirikisha wafanyabiashara toka mwaka jana na ujenzi huu unatarajiwa kuanza Julai, mwaka huu, baada ya serikali kutupatia fedha za kufanikisha ujenzi huu," alisema.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, viongozi wa soko hilo wakizungumza na waandishi wa habari, walidai kuwa wanapanga kufanya maandamano hadi Bungeni ili kufikisha kilio chao kwa Waziri Mkuu.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri (kushoto), akizungumza wakati wa futari iliyoandaliwa na Taasisi ya The Dodoma General Muslim Association (DGMA), iliyofanyika jijini Dodoma juzi jioni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Samia mgeni rasmi uhuru wa habari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari ambayo kitaifa yatafanyika Mei 3, mwaka huu jijini Arusha.

Kaimu Mkurungenzi Idara ya Habari (MAELEZO), Rodney Mbuya, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo ya habari Duniani.

Alisema katika siku hiyo pia kutakuwapo na utoaji wa tuzo za utambuzi wa umuhimu wa vyombo vya habari nchini.

Mbuya alisema tuzo hizo ni maalumu kwa ajili ya waandishi wa habari na wataalamu wa mawasiliano, vyombo vya habari na wamiliki wa vyombo vya habari

Vilevile, aliyataja makundi ya tuzo hizo kuwa ni tuzo za kijamii, sayansi na teknolojia, utalii na uwekezaji, wamiliki bora wa vyombo vya habari, michezo na burudani, mwandishi ajaye, mwanahabari mwanamke mwenye mafanikio katika tasnia ya habari, vyombo vya habari vya kidigitali, ushirikiano, malengo ya maendeleo endelevu na mtangazaji bora wa serikali na umma.

Akifafanua kuhusu tuzo za sayansi na teknolojia alisema ni maalum kwa ajili ya kampeni za uandishi wa habari na vyombo vya habari ambazo zimesawiri kwa ufanisi maendeleo ya bidhaa za kiteknolojia, maendeleo ya teknolojia mpya, miundombinu muhimu na teknolojia zinazochochea mabadiliko ya dijitali.

"Mshindi wa kategoria hii ni mwandishi wa habari au vyumba vya habari, tuzo hizo zitaonyesha mchango na thamani ya vyombo vya habari duniani na utaenziwa. Pia katika tuzo ya utalii mshindi ataonyesha uwezo wa kuandika stori na fursa ya kuwasilisha mvuto wa kipekee wa mahali alipotembelea au uzoefu wa safari," alifafanua

Kaimu Mkurugenzi huyo pia alisema kipengele cha wamiliki wa vyombo vya habari kuwa kitawatambua wamiliki waliotoa mchango mkubwa kwenye tasnia ya habari kupitia mipango bora ya maudhui ya vyombo vya habari, kampeni maalum, hafla au matangazo mengine yanayotokana na ushirikiano yaliyoibua fikra mpya na ubunifu katika nyanja ya habari.



# SACCOS yataka jamii kusaidia wagonjwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATANZANIA wameshauriwa kuwa na utamaduni wa kuwatembelea na kuwafariji wagonjwa wanaokuwa wamelazwa hospitalini ikiwa ni pamoja na kuwasaidia mahitaji mhimu ili kuwapunguzia maumivu na gharama za matibabu.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Wafanyakazi wa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) wanaofanya kazi kwenye Karakana ya Mbeya (MBESACCO), Brighton Mgeni, aliyesema hayo juzi jijini hapa wakati wanachama walipokuwa wanakabidhi msaada kwa wagonjwa.

Walikabidhi misaada mbalimbali kwa wagonjwa waliolazwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Kanda, Mbeya. Baadhi ya misaada iliyotolewa ni sabuni, mafuta ya kupakaa na dawa za miswaki.

Mgeni alisema walikabidhi msaada huo kutokana na uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Chama hicho ambao uliamua sehemu ya faida ambayo chama kilipata kwenye mwaka wa fedha uliopita, kutumia kuwafariji wahitaji.

Alisema Bodi ya SACCOS hiyo iliamua kutoa msaada kwa wagonjwa walioko kwenye hospitali hiyo kwa sababu ni miongoni mwa maeneo yenye uhitaji na kwamba wataendelea kutoa misaada hiyo kwenye maeneo mengine.

"Tunatoa rai kwa taasisi zingine zikiwamo zinazofanya shughuli kama za kwetu kujitahidi kuwaona wahitaji kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo hospitalini, majumbani na hata kwenye vituo vya kulelea watoto yatima," alisema Mgeni.

Meneja wa SACCOS hiyo, Damian Kaaya, alisema misaada ni sehemu ya utaratibu wa SACCOS kwa maelezo kuwa kuna kipengele ambacho kinawataka kusaidia jamii inayowazunguka kwenye shughuli zao.

Alisema kabla ya kutoa msaada huo walianzia kutoa msaada kwenye Shule ya Msingi Ikuti ambayo iko jirani na ilipo karakana ya TAZARA na kwamba wataendelea kutoa katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mbeya.

Muuguzi Mkuu Msaidizi wa Hospitali ya Kanda, Mercy Lutumo aliwashukuru wanachama wa MBESACCO kwa kuichagua hospitali hiyo kuwa sehemu ya kutoa msaada wao akidai kuwa wapo baadhi ya wagonjwa ambao huwa wanakosa mahitaji muhimu.

Alisema hospitali hiyo inapokea wagonjwa kutoka katika mikoa saba ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambao baadhi yao huwa wanakuwa hawana ndugu wa kuwasaidia na wengine wana ndugu lakini hawana uwezo mzuri kiuchumi.

Baadhi ya wagonjwa wanaopokewa katika hospitali hiyo, alisema hawana uwezo wa kumudu gharama, hivyo kuilazimu hospitali kuwasamehe na wengine husaidiwa na wasamaria wema kulipa gharama hizo.

"Tunawaalika na wadau wengine ambao wana uwezo waje wawasaidie wagonjwa wetu, tuna wagonjwa ambao wanatoka maeneo mbalimbali na wenye uwezo tofauti wa kiuchumi, kuna baadhi ya wagonjwa ambao huwa wanakuja hapa kwa dharura na kulazwa hasa wanaopata ajali, unakuta hana hata ndugu wa kumhudumia," alisema Lutumo.

Alisema wahitaji wapo pia katika maeneo mengine ya mkoa, hivyo akawataka wadau kwenda kuwasaidia pia akidai kuwa misaada ni miongoni mwa sadaka muhimu.



Muuguzi Mkuu Msaidizi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Marcy Lutumo (wa tatu kushoto), akipokea msaada wa vitu mbalimbali kutoka kwa viongozi wa chama cha kuweka na kukopa cha wafanyakazi wa karakana ya Shirika la Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), kwa ajili ya wagonjwa waliolazwa kwenye hospitali hiyo, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Waunga mkono anwani makazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI jijini Mbeya wamesema uwekaji wa anwani za makazi na barabara za mitaa kupewa majina, utasaidia kurahisisha mawasiliano na kwamba wageni watakuwa wanafika kwenye maeneo wanayotaka kufika bila kupotea.

Wananchi hao waliyasema hayo jana wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, ya kukagua uwekaji wa anwani hizo pamoja na usimikaji wa vibao vya majina ya barabara katika maeneo mbalimbali ya jiji la Mbeya.

Mmoja wa wananchi hao, Safari Shibada, mkazi wa Soko Matola, alisema katika baadhi ya maeneo ya jiji hilo ilikuwa vigumu kumwelekeza mgeni na akafika kutokana na kutokuwapo kwa alama maalumu.

Alisema kuna maeneo magari na vyombo vingine vya usafiri wa umma havifiki kwa hiyo hata kuwaelekeza wageni ilikuwa vigumu na kwamba kwa sasa baada ya kuwekwa majina ya barabara na nyumba kuwekwa namba itakuwa rahisi.

Shibanda alisema mambo hayo walikuwa wanayasikia tu kwenye vyombo vya habari kwamba kuna baadhi ya mataifa duniani yalianza siku nyingi kutumia utaratibu huo.

"Huu utaratibu ni mzuri sana na sisi tunaamini utatusaidia. Hili eneo letu la Soko Matola lilishapangwa miaka mingi lakini huu utambulisho umekuja kuyaongezea thamani zaidi," alisema Mwashibanda.

Naye Fanuel Chombo alisema mbali na uwekaji wa alama hizo kuwa na faida kwenye mawasiliano, pia zoezi hilo lilisaidia kuongeza ajira kwa vijana hasa awale walioshiriki kwenye uwekaji wa namba kwenye nyumba za wananchi na kuziingiza kwenye mfumo.

Alisema vijana wengi walinufaika na ajira hizo za muda na hivyo kujipatia kipato ambacho kitawasaidia kuendesha maisha yao na kwamba wengine wanaweza wakazitumia fedha walizozipata kama mitaji ya kuanzisha biashara.

Dk. Chuachua aliwataka wataalamu wanaotekeleza zoezi hilo hasa la kuweka majina ya barabara kuharakisha zoezi hilo ili kuwasaidia wananchi.

Alisema wanapojipatia barabara majina ya viongozi ni lazima wazingatie taratibu na waangalie aina ya viongozi wanaopewa barabara kwa kuangalia uandilifu na namna walivyosaidia jamiii.

# Wachimbaji madini wahamasishwa sensa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya imewataka wachimbaji wadogo wa madini kujiandaa kushiriki sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu nchini kote.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, aliyesema hayo juzi alipokuwa anazindua utoaji elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kushiriki kwenye sensa hiyo ambayo alisema kila mmoja anatakiwa kushiriki.

Alisema asilimia kubwa ya wachimbaji wadogo wilayani hapa wana tabia ya kuhamahama kutoka sehemu moja kwenda nyingine na kwamba endapo wataendelea na utaratibu huo, kuna uwezekano wasishiriki tukio hilo muhimu.

Kwa mujibu wa Mayeka, katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye jambo hilo, wananchi wote watakiwa kusitisha uhamaji ili wakutwe na maofisa wa sensa kwenye maeneo yao na wahesabiwe.

Alisema sensa ya watu na makazi ni muhimu kwa ajili ya kuisaidia serikali kupanga mipango ya kuwahudumia wananchi, hivyo akawataka kila mmoja kujiandaa kuhesabiwa.

"Hata wafugaji wetu mnatakiwa msihamehame katika kipindi hiki maana mnaweza mkaathiri sensa. Kila mmoja akutwe kwenye eneo lake ili ahesabiwe na hii itatusaidia pia kupata takwimu sahihi hata za wafugaji," alisema Mayeka.

Kadhalika, aliwataka wananchi kupuuzia upotoshaji unaoenezwa na baadhi ya watu kuhusu sensa wakihusisha na baadhi ya vitu ambavyo si sahihi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Tamim Kambona, alisema kwa sasa wanaendelea na maandalizi ya sensa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa viongozi wa ngazi mbalimbali kabla ya kuingia kwa wananchi.

Alisema wanawashirikisha viongozi wote wa serikali ngazi za chini, viongozi wa dini na viongozi wa mila ili na wao washiriki kwenye uhamasishaji wa wananchi wanaoishi nao kwenye maeneo yao.

Kambona aliwataka viongozi wote wa serikali ndani ya wilaya kushiriki kutoa elimu kwa wananchi ili mpaka kufika tarehe ya kuhesabiwa watu wote wawe na uelewa mzuri kuhusu sensa ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa.

"Wewe kama ni ofisa mtendaji wa kijiji, mwenyekiti wa kijiji, diwani na watumishi wengine lazima tushirikiane kwenye uhamasishaji. Tumieni mikutano ya kijiji na mikusanyiko mingine kuwakumbusha wananchi wajiandae," alisema Kambona.

Baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo, waliishukuru serikali kwa kuanza kutoa elimu mapema wakisema itawasaidia watu wote kujua umuhimu wa zoezi hilo na hatimaye kushiriki kikamilifu.

Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa wilaya za Mkoa wa Mbeya zenye shughuli zinazowahamasisha wananchi kuhamahama hasa shughuli za uchimbaji na ufugaji.





Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja, Abubakar Khamis Ali, akiwaonyesha waandishi wa habari mkoani humo jana, pikipiki iliyoibwa na kutumiwa na wahalifu katika matukio ya wizi na uporaji, baada ya kuwakamata watuhimiwa zaidi ya watano kwa matukio hayo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wazazi wafundwa malezi ya watoto

**Na Mwandishi Wetu**

MKE wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Zainab Kombo Shaib, amesema jamii inapaswa kuwasomesha watoto kwa malengo ya kupambana na soko la ajira ikiwamo kujiajiri baada ya kumaliza masomo.

Aliyasema hayo Mtambwe wilaya ya Wete Pemba, wakati akizungumza na wajasiriamali wanawake katika kuangalia namna bora ya kupambana na changamoto za kimaisha zinazowakabili.

Zainab alieleza mbinu zitakazowasaidia wanawake katika kuzilea familia na jamii kwa ujumla ikiwamo kuwajengea mazingira mazuri ya kimasomo watoto.

"Tunahitaji kukijenga kizazi chetu katika kupata elimu ambayo itawakomboa kimaisha na kujiajiri na ongezeko la uhitaji wa ajira za serikali ni kubwa," alisisitiza Zainab.

Nao viongozi wa vikundi hivyo vya ujasiriamali vya wanawake, walieleza changamoto zao zikiwemo mitaji na vitendea kazi sambamba na kuomba ushirikiano wa serikali katika kuzitatua.

Katika ziara yake hiyo, Zainab alikagua miradi ya wanakijiji ikiwamo ufugaji, kilimo na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na kinamama kama sehemu ya ujasiriamali katika vijiji vya Kisiwani kwa Binti Abeid, Wete Limbani, Kipangani na Selemu mkoa wa Kaskazini Pemba.

# Waziri apigia debe uwekezaji bahari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imewataka wananchi kuwekeza katika bahari kwa vile bado kuna fursa nyingi za kiuchumi ambazo hazijatumika.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, aliyasema hayo jana wakati akikagua ujenzi wa boti za uvuvi na ukulima wa mwani na mashamba ya majongoo bahari, Amani na kijiji cha Mangapwani.

Alisema serikali imepania kuwawezesha wajasiriamali wa mazao ya bahari kuvua, kulima na kufuga kwa njia za kisasa ili wapate tija na soko la uhakika.

Waziri huyo alisema wizara yake inategemea kukabidhi boti hizo zikiwa na vifaa vya kisasa kwa wavuvi na wakulima wa mwani Unguja na Pemba kwa wakati uliopangwa ili wananchi wafaidike na rasilimali za bahari zilizowazunguka.

Naye Meneja wa kampuni ya Qiro Group Company Ltd iliyopewa zabuni ya kutengeneza boti hizo, Makame Mchina, aliishukuru serikali kwa kuiamini kampuni yake kuipa tenda hiyo ambayo ameahidi kuikamilisha kwa wakati waliokubaliana.

Alisema kampuni yake imepewa tenda ya kutengeneza boti 250 ambazo zitakamilika mwanzoni mwa Mei, mwaka huu. Mkurugenzi wa kampuni ya kizalendo ya Ocean Enterprises, Khamis Rashid, iliyopewa tenda ya boti 50 alitoa wito kwa kampuni za kizalendo kujiamini na kuomba tenda zinazotolewa na serikali ili kuhakikisha kazi zote za serikali zinafanywa nchini hali itakayosaidia kuongeza ajira kwa wananchi.

Pia Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi alitembelea mashamba ya majongoo bahari yanayojengwa katika eneo la Mangapwani na kuahidi kuwa wizara itawatoa katika ufugaji wa kizamani ili wafuge kisasa na wapate tija.

# Mbaroni tuhuma kufanya uhalifu, utapeli

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, linawashikilia watu 12 kwa tuhuma za kufanya makosa yakiwamo wizi, utapeli na usambazaji wa taarifa za uongo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake, Mwembe Madema, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoani humo, Abubakar Hamis Ali, alisema matukio sita ya kuvunja vioo vya magari na kuiba vitu mbalimbali yameripotiwa na jeshi hilo likalazimika kufanya msako mkali na kuwakamata watuhumiwa.

Kamanda Abubakar alisema jeshi hilo linamshikilia Kassim Mbarouk Omar mkazi wa Chamanzi, Dar es Salaam, akiwa na vitu vilivyoibwa katika magari pamoja na pikipiki ambayo ilikuwa ikitumika kufanya matukio ya kihalifu.

Alisema mtuhumiwa huyo pia alikamatwa na komputa mpakato tatu, simu na vitu vingine zikiwamo fedha bandia. Baada ya mahojiano, alisema mtuhumiwa huyo alikiri kufanya matukio hayo na kueleza kuwa alishirikiana na mwezake ambaye ni Majid Khamis mkazi wa Chamanzi.

Kamanda huyo alisema jeshi liliunda kikosi maalum ambacho kilifika Dar es Salaam na kumkamata mtuhumiwa huyo nyumbani kwake, Chamanzi na baada ya upekuzi, alikutwa na vitu mbalimbali.

"Baadhi ya Wananchi wamefika kituo cha polisi na kutambua vitu vyao na watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani upelelezi utakamilika," alisema.

Pia kamanda huyo alisema jeshi la polisi pia limewakamata watuhumiwa sita ambao wanajihusisha na vitendo vya kitapeli katika maeneo mbalimbali Zanzibar na Tanzania Bara.

Alisema watu hao walikuwa wanawalaghai baadhi ya wananchi kwa kutumia mbinu kwamba wao ni wafanyabiashara wa madini na kuwashawishi kufanya nao biashara na kuwatapeli fedha.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, alisema Jeshi la polisi lilifanikiwa kuwakamata matapeli hao wakiwa na gari lenye namba za usajili Z.835 KB ambalo hutumika katika kutekeleza vitendo hivyo vya utapeli.

Aliwataja watuhumiwa wengine wa utapeli ni Farid Suleiman Ali, Othman Ali Hoza, Maryam Amani Mussa, Hassan Said Hassan, Said Kitwana Ali, Salome Geofrey Joseph, Sabri Mpenda Mahanda, Ahmed Ibrahim, Kombo Omar na Mohd Salum.

Pia alisema polisi wanamshikilia Ali Issa Makame mkazi wa Fuoni, Unguja, kwa tuhuma za kusambaza taarifa za uongo ambazo zinalengo la kulichafua jeshi la polisi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA ACADEMIC TRANSCRIPT



**GENTLE NGABANI MTENGA** anatangaza kupotea kwa **TRANSCRIPT OF DIPLOMA IN CIVIL ENGINEERING** chenye usajili namba 135101061 kilichotolewa na **NACTE** kupitia chuo cha **ST.JOSEPH UNIVERSITY** mwaka **2016.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: DAR/CHU/RB/141375/2022

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Deudedit gayombo Maige wa Bariadi simiyu atangaza kupotelewa kwa kadi yake ya pikipiki namba.Mc 910CNV,Aina ya Sinoray,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa -sm/Bar/rb/148674/2022

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA DISTRICT AT KYELA**

**CIVIL PROBATE CASE NO......1.........OF 2022**

**MARY TRANS MWAKIJALE MWAKITALU PETITIONER**

**VERSUS**

**LUGANO JOEL MWAKITALU.....RESPONDENT**

**TO LUGANO JOEL MWAKITALU OF KAJUNJUMELE ..IPONJOLA**

**TAKE NOTICE** that hearing of the above suit has been set down for Hearing on 10 day of **MAY 2022 at 08;30 am** in forenoon thereafter at the District Court.

You must produce on that day all the witnesses upon Whose evidence and all the document upon which you intend really in support of you case.

**Given under my hand and the seal of this court this 14 day of April 2022.**

DISTRICT COURT KYELA TANZANIA

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE

KYELA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU ELIBARIKI WILLIAM LOISHOOKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T985DWR** aina ya **TOYOTA TOWNACE**, Rangi Nyeupe yenye Chasis **No.KM75tC07245,** Engine **No.7K0847872.**Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha

Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DOD/DOD/RB/146878/2022**

**IN THE DISTRICT COURT IF SIMANJIRO AT ORKESUMET**

**CRIMINAL APPEAL NO 1 OF 2022**

**(CF Nyumba ya Mungu Primary Court in Criminal Case No.5 of 2022)**

**MOKIYA SANDIKOO.....APPELLANT**

**VERSUS**

**SAIDI MSHAMBA........ RESPONDENT**

**TO:SAIDI MSHAMBA**

**WHENEVER YOU ARE**

**WHEREAS,**the above named appellant has lodged an appeal against you before this court.

You are hereby summoned to appear in this court in person or by your advocate or agent duly authorized in 25th day of APRIL,2022 at 09:00 a.m before Hon O.I Nicodemo -RM to answer the appeal and you are directed to bring all documents upon which you wish to rely in support if your defence.

**TAKE NOTICE** that,in default if your appearance in that day before mentioned,the appeal shall be heard and determined in your absence.

GIVEN under my hand and the seal of this court 29th day of April 2022

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LANTRACK (T) COMPANY LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T596 DFP, CHASSIS NAMBA: LFNGBRJD7FAC02038, ENGINE NAMBA: 52557786.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

POLISI CONTROL NAMBA: **9910832382474**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA J/PC 54 (MCA/84)**

**Mahakama ya Mwanzo ya KAWE**

**Wilaya ya KINONDONI**

**MADAI NAMBARI 127 ya 2021**

**Mdai MANUMBU LADISILAUS na ASWELELA**

**Mdaiwa SAID KACHINGWE**

**Kwa SAID KACHINGWE**

**TOKYO GERAGE LAUND ABOUT DAR ES SALAAM**

**Kwa kuwa mdai/wadaiwa ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba/Eleza hapa habari ya mdai**

**UNATAKIWA KUFIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA SIKU YA TAREHE 19/04/2022 KWA KUJIBU MADAI YA PESA**

Kwa hiyo unahitajiwa mnahitajiwa kuudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMANNE tarehe 19/04/2022 saa 2.30 Asubuhi kwa kujibu madai haya. Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wake/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa hati hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Chama ya Mahakama hii leo tarehe 04/04/2022

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI

PASKAL KIHWELO anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI(TOYOTA VISTA) mali ya THE CATHOLIC DIOCESE OF IRINGA yenye namba za usajili T 428 BEZ

Chassis namba: ZZV500004961

Injini namba : 1ZZ0601490

Kadi Namba : 9115418

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***



***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***



**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA



Baadhi ya raia wakiondoka miji yenye mashambulizi ikiwamo Mariupol, nchini Ukraine, baada ya nchi hizo zinazohasimiana kukubaliana kufungua njia za kiutu.
**PICHA: BBC**

UCHAGUZI MKUU KENYA 2022:

## Wa Iria: Ninawania urais sitishwi na 'farasi' wawili

**Nairobi,** KENYA

GAVANA wa Murang'a, Mwangi Wa Iria, amesema hakuna kitakachomfanya aache azima yake ya kugombea urais kwenye uchaguzi mkuu ujao.

Wa Iria, ambaye alianza kampeni zake Jumatatu wiki hii, alipuuza wanaosema kwamba jamii ya Agikuyu haifai kuwa na mgombea urais, kwenye uchaguzi mkuu kwa sababu imetoa marais watatu tangu Kenya ilipopata uhuru.

Alisema kama Mkenya, ana haki ya kidemokrasia kugombea kiti chochote cha kisiasa na kwamba ni Wakenya watakaoamua atakayekuwa rais wao kwenye uchaguzi.

Akifanya kampeni katika kaunti ndogo ya Gatanga, Murang'a alisema kwamba ataomba watu wa eneo la Mlima Kenya, kumuunga mkono kama wagombea wengine wa urais wanavyoungwa mkono na jamii zao.

"Kuna zaidi ya wapigakura milioni nane katika eneo hili na nitaenda mashinani kujaribu kupata kura nyingi iwezekanavyo. Azma yangu sio ya kikabila bali ni mapenzi yangu ya kuhudumia Wakenya na kufufua uchumi unaodorora," alisema.

Wa Iria alisema kwamba kuanzia wiki ijayo, ataenda katika kaunti nyingine kutafuta uungwaji mkono na kupuuza wale wanaosema uchaguzi utakuwa kati ya farasi wawili, akitafsiriwa kuwalenga Raila Odinga na Naibu Rais William Ruto.

"Tufanye kampeni kwa amani na kujaribu kuepuka nadharia hii ya kwamba kutakuwa na farasi wawili kwenye uchaguzi mkuu ujao," alisema gavana huyo.

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# Russia, Ukraine zakubaliana maeneo salama ya kiutu

**Kyiv,** UKRAINE

IKIWA ni siku ya 57 tangu Russia ilipoanza mashambulizi dhidi ya Ukraine, pamoja na kutokubaliana baadhi ya masuala, jambo moja walilitayari kukubaliana na kufungua njia salama za kiutu.

Aidha, Kamanda wa Kikosi cha Wanamaji aliye katika kiwanda cha chuma cha Azovstal, Ukraine, Meja Serhiy Volyna, alisema tarehe ya mwisho imepita kwa wanajeshi wa Ukraine huko Mariupol kujisalimisha, akisema hii ndiyo hotuba yetu ya mwisho kwa ulimwengu. Huenda ikawa ni hotuba yetu ya mwisho."

Alisema wanajeshi wake hawatajisalimisha, ingawa aliomba msaada wa kimataifa. Meja Volyna aliongeza kwamba wanajeshi 500 waliojeruhiwa na mamia ya wanawake na watoto walikuwa kwenye hifadhi kando yao.

Ukraine ilisema kwamba makubaliano pekee na Russia, hadi jana, yalikuwa ni kwenye mji wa Mariupol kuruhusu njia ya kiutu, kwa ajili ya wanawake, watoto na watu wazima kondoka eneo hilo.

Naibu Waziri Mkuu alisema: Kwa kuzingatia hali mbaya ya kibinadamu huko Mariupol, hapa ndipo tutazingatia juhudi zetu," Iryna Vereshchuk alisema katika chapisho kwenye Facebook.

Wakati huo huo, Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Ulaya, Charles Michel ameitembelea Ukraine kwa ziara inayolenga kuonesha uungaji mkono kwa taifa hilo linalokabiliwa na vita tangu Russia ilipotuma vikosi vyake miezi miwili iliyopita. Michel alilakiwa mjini Kyiv na Naibu Waziri Mkuu wa Ukraine, Olga Stefanishyna, na anatarajiwa kukutana na Rais Volodymyr Zelensky wa Ukraine baadaye leo.

Ziara ya kiongozi huyo wa Umoja wa Ulaya inafanyika wakati serikali ya Ukraine imetangaza kufikia makubaliano na Russia ya kufungua ujia mpya za kuruhusu wanawake, watoto na wazee kuondoka kutoka katika mji uliozingirwa wa Mariupol.

**MSAADA KIJESHI**

Wakati huo huo, Ukraine, jana, imepokea ndege mpya za kijeshi kutoka kwa mataifa washirika kusaidia kuimarisha uwezo wake wa kujilinda wakati Russia inazidisha mashambulizi upande wa Mashariki ikilenga kulikamata jimbo la Donbas.

Wizara ya Ulinzi ya Marekani, imethibitisha kupelekwa kwa ndege za kivita Ukraine ingawa haikutaja idadi wala mataifa yaliyochangia msaada huo wa kijeshi. Ukraine, iliyaomba mataifa ya Magharibi kuipatia ndege aina ya MiG chapa 29s kwa sababu marubani wake wana uzoefu wa kuzirusha na mataifa mengi ya Mashariki mwa Ulaya yanamiliki ndege hizo.

Uamuzi wa kuipatia Ukraine ndege za kivita ni sehemu ya juhudi za hivi karibuni kabisa za mataifa ya Magharibi kujibu operesheni kali inayofanywa na Russia.

Serikali ya Norway ilisema, imeipatia Ukraine takriban makombora 100 aina ya Mistral, yaliyotengenezwa na Ufaransa na yenye uwezo wa kudungua ndege.

Canada pia ilisema itatuma silaha nzito Ukraine, ila haikutoa maelezo zaidi.

Rais wa Marekani Joe Biden naye kupitia Msemaji wa Ikulu ya White House, Jen Psaki alisema msaada wa kiusalama, kiuchumi na kiutu kwa Ukraine ni mambo yatakayozingatiwa.

Viongozi hao watatu mapema Jumanne wiki hii, walizungumza na viongozi wengine wa Magharibi ili kushirikiana katika kuyajibu mashambulizi ya Russia, Mashariki mwa Ukraine.

Vyombo vya habari vya Marekani vinasema nchi hiyo itaidhinisha msaada wa kijeshi wa dola milioni 800 kwa ajili ya Ukraine.

Msaada huo unakuja chini ya wiki moja tu baada ya msaada mwingine wenye thamani sawa na kiasi hicho cha fedha kuidhinishwa kwa ajili ya nchi hiyo.

**UN**

Katika kipindi cha chini ya miezi miwili, tangu wanajeshi wa Russia walipoanza mashambulizi Ukraine, raia takribani milioni tano wa Ukraine wameondoka nchini mwao.

Pia, inakadiriwa milioni saba wamekoseshwa makazi ndani ya nchi kwa mujibu wa Shirika la Kuhudumia Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR).

Wakimbizi wengi wa Ukraine wametafuta hifadhi katika nchi jirani za Ulaya ambako wanapewa ulinzi wa muda na huduma mbalimbali.

Wa-Ukraine sasa ni kundi kubwa la pili la wakimbizi duniani wa pili baada ya wakimbizi zaidi ya milioni 6.8 wa Syria na wameongeza jumla ya idadi ya wakimbizi duniani hadi karibu milioni 32. Vita hivyo pia vimewafanya watu milioni 7.1 wa Ukraine kuwa wakimbizi ndani ya nchi hiyo, idadi kubwa zaidi ya wakimbizi wa ndani inayohusishwa na migogoro duniani.

Vita vya Ukraine vimechochea mojawapo ya matukio ya kuhama kwa watu na matatizo ya kibinadamu yanayokua kwa kasi kuwahi kutokea.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres alitoa wito wa kusitishwa kwa mapigano hayo, ili kutoa nafasi ya wiki takatifu ya Wakristo wa dhehebu la Orthodox akidai wanakaribia kuadhimisha Sikukuu ya Pasaka.

**ITALIA YAFUATA GESI, MAFUTA AFRIKA**

Kutokana na mgogoro kati ya Russia na Ukraine, Italia imeamua kuwatuma mawaziri wake wawili, barani Afrika kwa ziara ya kutafuta mikataba mipya ya nishati.

Hatua ya Italia kuhangaikia suala hilo ni kujinasua na matumizi ya gesi kutoka Russia.

Waziri Mkuu wa Italia, Mario Draghi analenga kuyatumia mataifa mawili ya Angola na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kama wasambazaji mbadala wa nishati ya Russia, inayofikia asilimia 45 ya gesi yote inayotumika nchini Italia.

***• Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao***

HABARI MICHEZO

# Serikali, TSA waipongeza timu ya Taifa ya Kuogelea

Na Mwandishi Wetu

BARAZA la Michezo la Tanzania (BMT) na Chama Cha Kuogelea (TSA), wamewapongeza timu ya Taifa ya mchezo wa Kuogelea ya Tanzania kwa matokeo mazuri waliyopata katika mashindano ya Kanda ya Nne Afrika yaliyomalizika hivi karibuni mjini Lusaka, Zambia.

Tanzania iliwakilishwa na jumla ya waogeleaji 18 katika mashindano hayo yaliyoshirikisha nchi nyingine 13 ambapo waogeleaji wa Tanzania walishinda jumla ya medali 13, nne zikiwa ni za dhahabu, nne za fedha na tano za shaba.

Muogeleaji chipukizi, Filbertha Demello (12), ameshinda jumla ya medali sita, tatu zikiwa ni za dhahabu, moja fedha na mbili za shaba.

Filbertha, ambaye anatokea Klabu ya Bluefins, pia ameshinda kikombe cha mshindi wa tatu kwa waogeleaji wenye umri wa miaka 12. Nahodha wa timu hiyo, Collins Saliboko ambaye anatokea klabu ya Dar Swim Club (DSC), ameshinda medali moja ya dhahabu, moja ya fedha na mbili za shaba.

Muogekeaji mwingine, Mark Tibazarwa wa DSC, ameshinda medali tatu ambapo mbili ni za fedha na moja ya shaba.

Mbali ya kushinda medali, waogeleaji wa Tanzania pia waliweza kuimarisha muda (PBs), katika mashindano hayo yaliyoshirikisha nchi nyingine 13. Waogeleaji wengine wa Tanzania walioshiriki katika mashindano hayo ni Julius Missokia, Mischa Ngoshani, Mahek Desai, Michael Joseph, Austin Okore, Sarah Tibazarwa na Salman Yasser. Wengine ni Muskan Gaikwad, Isaac Mukani, Aminaz Kachra, Lina Goyayi, Enrico Barretto, Maryam Ipilinga, Delbert Ipilinga na Ethan Alimanya.

Afisa michezo wa Baraza la michezo Tanzania (BMT), Halima Bushiri, alisema kuwa waogeleaji hao wameweza kuitangaza vema nchi nje ya mipaka yake na kuleta heshima katika mashindano ambayo Tanzania ilialikwa na kufanikiwa kusanya jumla ya pointi 902, hivyo kushika nafasi ya tisa.

"Matokeo yametufanya kujivunia kwani Tanzania iliwakilishwa na waogeleaji chipukizi ambao wameweza kufanya vema pamoja na kuwa na umri mdogo. Hii ni ishara kuwa mchezo wa kuogelea unazidi kupata maendeleo na mafanikio," alisema Halima.

Mwenyekiti wa TSA, Imani Alimanya, pia aliwapongeza waogeaji hao kwa matokeo na kushinda medali huku wengine wakiweka muda mpya.

Alimanya alisema wanaamini kuwa muda si mrefu, waogeleaji wa Tanzania wataweza kufanya vema katika mashindano ya Dunia, Olimpiki na Jumuiya ya Madola.



Waogeleaji wa Tanzania, makocha na viongozi wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kuwasili Uwanja wa Julius Nyerere (Terminal -3), wakitokea Zambia ambapo walishiriki katika mashindano ya Kanda ya Nne ya Afrika na kushinda medali 13. **MPIGAPICHA WETU**

# KUNDI LA STARS KUFUZU AFCON 2023 NI GUMU ASEMA MWAMBUSI

Na Adam Fungamwango

KOCHA mkongwe nchini, Juma Mwambusi, amefunguka baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuipanga timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kwenye Kundi F, katika kinyang'anyiro cha kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, mwakani nchini Ivory Coasta, akidai kuwa ni gumu, hivyo jitihada kubwa zinatakiwa kufanyika ili kufuzu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kocha huyo wa zamani wa Mbeya City, Yanga na Azam FC, alisema ukilitazama haraka unaweza kudhani ni kundi jepesi, lakini kiuhalisia ni gumu na kutaka jitihada kubwa kufanyika, ikiwamo maandalizi kabambe pamoja na kucheza mechi za kirafiki nyingi na timu za Afrika Kaskazini, maarufu kama za 'Waarabu'.

"Hakuna timu rahisi, zamani ikiandikwa Niger inasemwa haina kiwango, lakini kwa sasa wako vizuri kimiundombinu ya soka na wana wachezaji wengi wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi yao tofauti na sisi, kwa hiyo ni kundi gumu. Inahitajika jitihada kubwa kuhakikisha tunaweza kufanya lolote, mimi naamini kwa vijana wetu kama wakiweza kujitambua tunaweza kupita," alisema kocha huyo.

Alisema tayari makundi yameshatangazwa, hivyo maandalizi yanatakiwa yaanze sasa pamoja na mechi nyingi za majaribio.

"Tukiwatumia wachezaji wanaocheza nje ya nchi ambao nimewaona kwenye mechi zilizopita, wanaweza kutusaidia, ligi yetu kwa sasa ina ushindani, lakini tunahitaji mechi za majaribio nyingi na tucheze na timu za Afrika Kaskazini na mataifa yaliyoendelea kisoka na pia tupate mechi ambazo tutacheza ugenini, siyo kila mechi ya kirafiki tunacheza hapa hapa, haitatusaidia," alisema.

Stars imepangwa kwenye Kundi F na timu za Algeria, Uganda na Niger, ambapo timu mbili za juu zitafuzu moja kwa moja kucheza fainali hizo za AFCON nchini Ivory Coast mwakani.

## 'Mtoko wa Kibingwa' bado mashabiki wa4

Na Saada Akida

WAKATI homa ya mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga ikizidi kupamba moto, mashabiki wanne wamesalia kufikisha idadi ya mashabiki 24 watakaoshuhudia bure mchezo huo wa Aprili 30, mwaka huu.

Mechi hiyo la watani wa jadi, 'Kariakoo Derby' ambayo ni ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara, itapigwa katika Dimba la Benjamin Mkapa.

Kuelekea mechi hiyo, Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya Betika, imeandaa shindano la 'Mtoko wa Kibingwa' kwa kutoa fursa kwa mashabiki 24 kushuhudia mchezo huo wa Kariakoo Derby bure.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja Masoko wa Kampuni ya Betika, Nelson Mwanuzi, alisema mchatako wa kutafuta washindi unaendelea na wamebakiza nafasi ya watu wanne ili kukamilisha idadi ya mashabiki 24 ambao watalipiwa gharama zote na kampuni hiyo ikiwa ni pamoja na malazi, chakula na mahitaji yote muhimu.

"Wiki iliyopita droo ya 'Mtoko wa Kibingwa' ilipata mabingwa wengine, ambao wameungana na wale wa awali wenye tiketi mkononi za kushuhudia mchezo huo, Aprili 29, washindi wote watawasili Dar es Salaam kushuhudia mtanange huo wa Simba na Yanga," alisema Mwanuzi.

Aliwataja washindi sita wa wiki hii kuwa ni Dismas Chiloma (Dodoma), Aaron Kulinga (Mbeya), Emmanuel Kivambe (Shinyanga), Boniface Molel (Manyara), Shafii Mgomi (Mtwara) na Raphael Kibifu (Tabora).

## Sugu kuzindua Maisha na Muziki

Na Sabato Kasika

RAPA mkongwe wa muziki wa Hip hop, Joseph Mbilinyi 'Sugu', amesema, anatarajia kuzindua rasmi kitabu kinachoelezea maisha yake mwezi ujao.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, msanii huyo alisema, kitabu hicho amekipa majina mawili ya 'Muziki na Maisha' na 'From the Street to the Parliament' kwa sababu maalum.

"Sababu ya majina hayo mawili ni kwamba kinaelezea maisha yangu ya umachinga, muziki na pia hatua niliofikia ya kuwa mwakilishi wa wananchi wa Mbeya mjini kama mbunge wao," alisema Sugu.

Akifafanua zaidi, msanii huyo alisema, alitoa kitabu hicho mwaka 2012 bila uzinduzi na kwamba kiliishaka, na sasa amekichapisha upya baada ya mahitaji kuwa mengi na ameamua kuandaa uzinduzi rasmi.

"Uzinduzi wa kitabu changu utafanyika Mei 3, mwaka huu na nina mpango na kukitafsri kwa lugha ya Kiingereza ili mashabiki wangu wa nje ya nchi waweze kujua historia ya maisha yangu," alisema.

## ZISIKUPITE

### STERLING ATAKIWA MILAN

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27, yuko kwenye orodha ya wachezaji ambao AC Milan inataka kuwasajili huku kukiwa na ripoti za ununuzi wa timu hiyo ambayo ni bingwa mara 18 nchini Italia kwa dau la paundi milioni 850. (***Gazzetta dello Sport via Mail***)

### BARCA, REAL KWA RUDIGER

REAL Madrid na Barcelona wanataka kumsajili beki wa Chelsea na Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake unamalizika mwisho mwa msimu huu, lakini anataka kusalia Stamford Bridge. (***The Athletic***)

### SALIBA KUSALIA ARSENAL

MLINZI wa Arsenal na Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 21, amesema kuna uwezekano huenda akasalia Marseille kwa mkopo hata baada ya msimu huu kumalizika. (***Le Parisien***)

### TORRES AWINDWA UNITED

MANCHESTER United wamefufua nia yao ya kumsajili beki wa Villarreal na Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 25 msimu huu. (***Manchester Evening News***)

### MATIC HUYOOO ROMA

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho anapania kumleta Nemanja Matic katika klabu ya AS Roma baada ya kiungo huyo wa kati mwenye umri wa miaka 33, kutangaza kuwa anahama Old Trafford (***Tuttomercatoweb***)

### KANE KUBAKI TOTTENHAM

KLABU ya Tottenham ina imani ya kubaki kwa mshambuliaji Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, msimu huu wa majira ya joto. (***Mail***)

### NUNEZ HAITAKI NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle itarajiwa kusitisha nia yao ya kumnunua Darwin Nunez wa Benfica mwenye umri wa miaka 22, huku mshambuliaji huyo wa Uruguay akitaka kujiunga na klabu itakayocheza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. (***Telegraph***)

### NKUNKU NA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United italazimika kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa wanataka kumsajili mshambuliaji wa RB Leipzig na Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24.

### NKETIAH KUONDOKA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 22, anataka kucheza mara kwa mara katika kikosi cha kwanza na amehusishwa na klabu za Leeds, Crystal Palace na West Ham. (***The Beautiful Game Podcast***)

### EDWARDS AWINDWA RIGHTON

KLABU ya Brighton imeanza mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Khayon Edwards mwenye umri wa miaka 18, ambaye amefunga mabao 17 na kutoa pasi za mabao sita katika mechi 22. (***Mirror***)

### ZANIOLO ATAKIWA SPUR

TOTTENHAM Hotspur wanataka kumsajili kiungo wa kati wa Roma na Italia, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 22. (***Calciomercato***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RANGNICK AKIRI MAMBO MAGUMU MAN UNITED

**●●● Timu inahitaji kujengwa upya, kwangu ni wazi watakuwa wachezaji sita, saba, nane, labda 10 wapya...**

**LIVERPOOL,** ENGLAND

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick amedokeza kwamba kunaweza kuwa na uhitaji wa kusajili wachezaji kumi wapya baada ya kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Liverpool, Jumanne usiku.

Mchezo ulikamilika baada ya dakika 25 huku Liverpool wakiwa tayari wameibuka na ushindi wa mabao 2-0 na United hawakuwa na uwezo wa kurudi mchezoni.

Rangnick alibainisha kuwa United inahitaji kufanya marekebisho ya muda mrefu sawa na Liverpool na Manchester City.

"Ukiangalia klabu mbili ambazo kwa sasa zinatawala Ligi Kuu, zilifanya hivyo," alisema baada ya mechi.

"Wameleta makocha wawili na si tu wakaleta makocha, pia walibadilisha mambo yote kwenye mfumo, wanahitaji wachezaji wa aina gani, tunataka kucheza soka la aina gani?

"Kichwa cha habari cha kila kitu kilikuwa 'tunataka kucheza vipi?' Na chini ya kichwa hiki cha habari baada ya kila dirisha la uhamisho, waliunda timu waliyonayo katika klabu zote mbili.

> **"Timu inahitaji kujengwa upya, si kwa sababu wachezaji wengine lazima waende, lakini wachache hawana mikataba tena, mi kataba yao inaisha, basi kwangu ni wazi watakuwa sita, saba, nane, labda wachezaji 10 wapya."**

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 63, aliendelea kuimarisha pengo la kina la kikosi na usawa kati ya United na Liverpool ambapo matokeo ya Jumanne yalibadilika.

Ingawa Fred, Cristiano Ronaldo na Raphael Varane walikuwa miongoni mwa waliokosekana kwa 'Mashetani Wekundu' hao, Rangnick pia alibainisha kuwa Liverpool chini ya Jurgen Klopp aliyewasili hapo Anfield mwaka 2015 ni bora sana.

"Simlaumu mtu yeyote, si wachezaji wangu au mtu mwingine yeyote, lakini lazima tutambue ni aina gani ya kikosi walichokuwa nacho.

"Angalia benchi lao, angalia wachezaji wanne ambao hata hawakuwa kwenye kikosi: Roberto Firmino, Oxlade-Chamberlain hakuwapo kikosini, Minamino hakuwapo kikosini, Harvey Elliott hakuwapo kikosini.

"Hii inaonesha ni aina gani ya ubora na timu waliyoijenga kwa pamoja wakifanya kazi na Jurgen na timu yake.

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,171,

MECHI KALI

REAL SOCIEDAD
VERSUS
BARCELONA

1 | 3.10
X | 3.35
2 | 2.23

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HAALAND KUAMUA HATMA YAKE



**DORTMUND,** Ujerumani

UNAPOMZUNGUMZIA Erling Haaland, unazungumzia klabu tatu (kwa sasa), ni jukumu lake kuamua hatma yake msimu ujao.

Kimkataba, Haaland anaweza kuondoka Borussia Dortmund mwishoni mwa msimu huu na hilo litawezekana kwa klabu yeyote itakayolipia ada ya pauni milioni 63 ambayo ipo kwenye mkataba wake na klabu hiyo.

Japokuwa, hii haimaanishi kuwa Dortmund hawawezi kumbakiza klabuni hapo, lakini wanaweza kumshawishi mshambuliaji huyo kubakia Signal Iduna Park. Kwa hali ilivyo, Dortmund wanakwama kwenye hesabu zao sokoni.

Manchester City inaripotiwa kufikia makubaliano ya awali na Haaland na kwamba, City wanajiandaa kulipa fedha inayotakiwa kumsajili mchezaji huyo.

Pamoja na City, Real Madrid wanatajwa kwenye kinyang'anyiro hiki, ingawa kuna tatizo kidogo.

Uongozi wa klabu hiyo haufikirii kufanya usajili wa mchezaji yeyote ambaye matakwa yake ya mshahara yanaweza kuondoa usawa wa mishahara kwa wachezaji wao.

Kwa sababu hii, kuna uwezekano wakaachana na Haaland na kusajili mshambuliaji wa aina nyingine.



## *Bayern wamepanga bei ya Lewandowski*

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich tayari wamepanga bei yao kwa Robert Lewandowski, hii ni kwa mujibu wa Kicker kupitia Mundo Deportivo.

Wanadai kuwa klabu hiyo ya Bavaria inataka ada isiyopungua euro milioni 40 kwa mshambuliaji wao wa thamani kutoka Poland.

Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, ana mkataba na Bayern unaofikia kikomo msimu wa majira ya joto wa 2023 na msimamo rasmi wa klabu ni kwamba atakamilisha mkataba wake na wanafanyia kazi suala la kuongeza zaidi.

Suala la mkataba mpya linaweza kuwa changamoto na Bayern wanachelewa kuongeza mikataba ya wachezaji wenye umri zaidi ya miaka 30 kwa zaidi ya miaka miwili.

Kwa kuzingatia hilo Barcelona wamehusishwa na uhamisho wa staa huyo.

'La Blaugrana' hao wana nia ya kumpata namba tisa wa kiwango cha juu baada ya kushindwa kumpata Erling Haaland, hivyo wanaweza kwenda kwa Lewandowski.

## HABARI MICHEZO


,243,460

# JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/04/22 | 17:00 | Leicester vs Aston Villa | 2.63 | 3.28 | 2.53 |
| 02. 23/04/22 | 17:00 | Hull City vs Reading | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 03. 23/04/22 | 17:00 | Birmingham vs Millwall | 2.78 | 3.08 | 2.53 |
| 04. 23/04/22 | 17:15 | Fuenlabrada vs Ponferradina | 2.57 | 3.16 | 2.67 |
| 05. 23/04/22 | 20:30 | Adana Demirspor vs Trabzonspor | 2.40 | 3.39 | 2.74 |
| 06. 23/04/22 | 21:00 | Waalwick vs PEC Zwolle | 2.46 | 3.07 | 2.87 |
| 07. 23/04/22 | 21:30 | St. Pauli vs SV Darmstadt | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 08. 24/04/22 | 16:00 | Burnley vs Wolverhampton | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 09. 24/04/22 | 16:00 | Bologna vs Udinese | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 10. 24/04/22 | 16:00 | Metz vs Brest | 2.98 | 3.22 | 2.33 |
| 11. 24/04/22 | 17:15 | UD Ibiza Eivissa vs Las Palmas UD | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 12. 24/04/22 | 18:30 | Hertha BSC vs Stuttgart | 2.73 | 3.22 | 2.48 |
| 13. 24/04/22 | 21:45 | Lazio vs AC Milan | 2.78 | 3.27 | 2.41 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 21/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1968 | Bangkok Glass vs Ceres FC | 1.18 | 6.08 | 11.76 |
| 14:00 | 3453 | Shandong Luneng vs Lion City Sailors | 43.65 | 11.64 | 1.01 |
| 17:00 | 2508 | Melbourne City vs Jeonnam Dragons | 1.55 | 3.80 | 5.26 |
| 17:00 | 2890 | Daegu vs Urawa Red Diamonds | 3.99 | 3.55 | 1.76 |
| 17:00 | 4240 | Kawasaki Frontale vs Johor Darul Takzim | 1.46 | 4.00 | 6.04 |
| 17:00 | 4562 | Adanaspor vs Samsunspor | 3.06 | 3.31 | 2.12 |
| 17:30 | 1875 | Unirea Slobozia vs Hermanstadt | 6.02 | 3.50 | 1.54 |
| 18:00 | 1144 | Enyimba vs Kano Pillars | 1.30 | 4.39 | 9.76 |
| 18:00 | 1674 | Sunshine Stars FC vs Rivers United FC | 1.87 | 3.12 | 4.09 |
| 18:00 | 2524 | Montana vs PFK Sportist Svoge | 1.49 | 3.65 | 6.43 |
| 18:00 | 2828 | Akwa United vs Nasarawa United | 1.29 | 4.47 | 9.72 |
| 18:00 | 4074 | Heartland FC Owerri vs Plateau United | 2.78 | 2.73 | 2.68 |
| 18:00 | 5752 | MFM FC vs Wikki Tourist | 1.92 | 3.11 | 3.89 |
| 19:00 | 3502 | CSKA Sofia vs Slavia Sofia | 1.51 | 4.00 | 5.27 |
| 19:00 | 5878 | Flora II-Ida vs Virumaa FC Alliance | 1.55 | 4.51 | 4.91 |
| 19:00 | 5918 | Fremad Amager vs Hobro | 2.30 | 3.21 | 2.83 |
| 19:30 | 5408 | PAOK vs Olympiakos | 2.35 | 3.02 | 2.92 |
| 19:30 | 5890 | Magallanes vs Arturo Fernandez Vial | 1.66 | 3.35 | 5.04 |
| 20:00 | 1232 | Degerfors vs Hammarby | 4.18 | 3.84 | 1.66 |
| 20:00 | 2269 | Levante vs Sevilla FC | 3.40 | 3.35 | 2.10 |
| 20:00 | 3430 | IFK Varnamo vs Malmo | 5.62 | 3.97 | 1.49 |
| 20:00 | 3566 | Espanyol vs Rayo Vallecano | 2.44 | 3.10 | 2.95 |
| 20:00 | 4321 | Yverdon vs Sport FC-St. Gallen | 4.38 | 3.79 | 1.64 |
| 20:00 | 5916 | Helsingborg vs Elfsborg | 3.42 | 3.42 | 1.94 |
| 20:30 | 5004 | Eyupspor vs Boluspor | 1.72 | 3.56 | 4.19 |
| 20:45 | 4445 | FC Lugano vs FC Luzern | 2.12 | 3.26 | 3.11 |
| 21:00 | 1523 | Cadiz CF vs Athletic Bilbao | 3.15 | 3.00 | 2.39 |
| 21:00 | 5500 | Mushuc Runa vs CSD Macara | 2.74 | 3.08 | 2.44 |
| 21:10 | 2035 | Bodo Glimt vs Viking | 1.56 | 3.98 | 4.76 |
| 21:15 | 2232 | AL Musanaa vs Nizwa | 1.63 | 3.45 | 5.05 |
| 21:15 | 2885 | Muscat Club vs Saham Club | 2.01 | 3.16 | 3.50 |
| 21:15 | 3299 | Luka Koper vs NK Celje | 1.91 | 3.46 | 3.46 |
| 21:15 | 3407 | Al Nasr Salalah vs Sohar Club | 1.51 | 3.60 | 6.24 |
| 21:15 | 3551 | Bahla vs AL Etihad | 2.17 | 2.86 | 3.44 |
| 21:15 | 4625 | Al Suwaiq vs Oman Club | 2.08 | 2.91 | 3.64 |
| 21:15 | 4663 | Dhofar Salalah vs Al Nahda (Oman) | 1.66 | 3.35 | 5.04 |
| 21:15 | 4993 | Al Seeb vs Rustaq Club | 1.49 | 3.74 | 6.22 |
| 21:30 | 3367 | AL Badii vs Muharraq SC | 3.45 | 3.25 | 1.99 |
| 21:30 | 3767 | Najma Manama vs Al Hidd Club | 2.77 | 3.25 | 2.32 |
| 21:30 | 3984 | Al Ahli Manama vs Al Hala Muharraq | 2.29 | 2.92 | 3.12 |
| 21:45 | 4619 | Burnley vs Southampton | 2.66 | 3.26 | 2.52 |
| 22:00 | 3236 | Sarmiento Junin vs Defensa Justicia | 3.74 | 3.31 | 1.89 |
| 22:00 | 5676 | AL Tadamon vs AL Nasr | 3.99 | 3.65 | 1.74 |
| 22:15 | 4089 | Porto vs Sporting Lisbon | 1.84 | 3.41 | 3.80 |
| 22:15 | 5281 | SC Faetano vs SP Cailungo | 1.20 | 5.44 | 11.66 |
| 22:15 | 5670 | SS Pennarossa vs SS Cosmos | 1.07 | 7.59 | 29.20 |
| 22:15 | 5771 | SS Virtus vs SS Murata | 1.45 | 3.83 | 6.79 |
| 22:30 | 1419 | Nautico PE vs Retro FC Brasil | 2.34 | 2.77 | 3.21 |
| 22:30 | 2057 | Real Sociedad vs Barcelona | 3.10 | 3.35 | 2.23 |
| 22:30 | 2391 | Gremio vs Guarani SP | 1.54 | 3.65 | 5.65 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# MIL. 11/- ZA JACKPOT BONUS SPORTPESA ZAENDA TEGETA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Tegeta, Namanga jijini Dar-es-Salaam, Alex Stanley Mtui, ameshinda Sh. 11,350,818 kwenye Jackpot Bonus ya Sportpesa iliyochezwa mwishoni mwa wiki iliyoisha, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya 13.

**Akizungumza baada ya hafla ya makabidhiano ya hundi katika ofisi za Sportpesa jijini Dar es Salaam, Alex alisema alianza kucheza na Sportpesa miaka kadhaa iliyopita kabla ya wiki iliyopita kushinda dau lake kubwa.**

"Sikumbuki vizuri, lakini nilianza kucheza na Sportpesa miaka michache iliyopita, baada ya kuwa naona matangazo ya washindi kwenye mitandao ya kijamii. Mara nyingi ninapokuwa huru huwa natembelea mitandao, hivyo nilikuwa naona washindi wakitangazwa kila wiki," alisema.

Akielezea namna alivyopata ushindi huo wa Jackpot Bonus, alisema huwa anaweka mikeka mitatu mpaka minne kila wiki. Alafu mimi nacheza Jackpot zaidi, hivyo ikifika Alhamisi au Ijumaa huwa naangalia kiasi kilicho kwenye akaunti yangu ya Sportpesa kisha naweka.

Aliendeliea kufunguka kuwa aliweka mikeka mitatu kuanzia Jumatano, Alhamisi na wa mwisho aliweka Ijumaa. "Nilichambua kwa siku tatu na baadaye Ijumaa niliweka mkeka huu ulioshinda," alisema.

Alisema kuwa alijua kashinda Jumapili kwani aliangalia mechi ya mwisho ya Real Madrid dhidi ya Sevilla. "Nilikuwa mtaani kwangu na vijana tuna angalia mpira hii mechi ya Real Madrid. Wakati huo presha ilikuwa juu baada ya Sevilla kutangulia kufunga magoli mawili, lakini nashukuru Mungu Madrid walirudisha na kuongeza la ushindi, hivyo kunipa mimi nafasi ya kufikisha mechi 12 kwenye Jackpot Bonus".

Alex alihitimisha kwa kueleza kuwa pesa alizoshinda ataongeza kwenye mtaji wake wa biashara. "Sitakuwa na vitu vingi vya kufanya zaidi ya kuongeza kwenye mtaji wangu".

Akizungumza kwa niaba ya Sportpesa, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Sabrina Msuya, amempongeza Alex kwa ushindi huo wa Jackpot Bonus na kuwataka Watanzania kuipambania Jackpot kubwa.

"Kwa sasa Jackpot imepanda sana, hivyo nawaomba muendelee kucheza pamoja na mambo mengine mtumie fursa iliyopo kucheza multibet pamoja na Jackpot yenyewe, kwa wiki hii Jackpot ni Tsh. 1,171,243,460," alisema.




Mshindi wa SportPesa Jackpot Bonus, Alex Stanley, kutoka Tegeta, Dar es Salaam, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 11.3 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot inayoshindaniwa wiki hii ni Sh. 1,171,243,460. **PICHA: SPORTPESA**

# Mayanga asema kazi bado ngumu Mtibwa

**Na Mwandishi Wetu,** Morogoro

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Salum Mayanga, amesema licha ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma mwishoni mwa wiki, bado wana kazi ya kufanya ili kuzidi kusogea juu ya msimamo.

Mtibwa Sugar imefikisha pointi 23 ikipanda hadi nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa imeshinda michezo mitano, sare nane na imepoteza mechi saba, wakati matokeo hayo yanaifanya Dodoma Jiji kushuka hadi nafasi ya 14 na pointi 20 baada ya michezo 20.

Mayanga, alisema ulikuwa mchezo mzuri kwa kila timu kujitahidi kutengeneza nafasi ya kufunga, lakini anawapongeza wachezaji wake kwa ushindi walioupata kwani kila timu iliingia uwanjani ikihitaji matokeo ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Ulikuwa mchezo muhimu kwetu tulihitaji pointi tatu ili kuendelea kujiweka katika mazingira mazuri, tuliingia kwenye mchezo huu kwa ari, vijana wangu waliopata nafasi wameonesha uwezo mkubwa," alisema Mayanga.

Naye Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Masoud Djuma, alisema hajafurahishwa na matokeo hayo na kwamba makosa waliyofanya yamewaadhibu, lakini pia kushindwa kutumia nafasi walizopata kumewafanya wapoteze, hivyo nguvu zao wanazihamishia katika mchezo ujao.

Michezo
Alhamisi Aprili 21, 2022
Nipashe



## Haaland kuamua hatma yake

UKURASA 22

TUTAPAMBANA...



Wachezaji wa Simba; kutoka kushoto ni Gadiel Michael, Kennedy Juma na Henoc Inonga 'Varane', wakiwa mazoezini. Timu hiyo itashuka dimbani nchini Afrika Kusini Jumapili wiki hii kuvaana na Orlando Pirates kwenye mechi ya robo fainali mkondo wa pili wa Kombe la Shirikisho Afrika baada ya ile ya awali Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kushinda bao 1-0. **PICHA: MAKTBA**

## Paulsen: Stars ipo tayari kufuzu AFCON

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa, Taifa Stars, Kim Paulsen amesema kuwa wapo tayari kwa michuano ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, itakayofanyika nchini Ivory Coast.

Akizungumza baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kutoa droo ya michuano hiyo na timu ya Taifa ya Tanzania kupangwa kwenye Kundi F na timu za Algeria, Uganda na Niger, amesema ukiwepo uwajibikaji wa pamoja, huku kila mtu akifanya wajibu wake, kuanzia viongozi, benchi la ufundi na wachezaji, inawezekana kwa Tanzania kufuzu kwenye michuano hiyo.

"Nadhani kwa sasa tunasubiri ratiba, lakini Algeria ni timu kubwa kama zilivyo Morocco, Tunisia na nyingine, Uganda ni timu nzuri ambayo wametuzidi kwenye viwango vya soka, Niger sijui sana habari zao, lakini mechi zitakuwa ngumu, kila mtu sasa ana wajibu kuanzia viongozi, benchi la ufundi na wachezaji ili tufuzu AFCON, kifupi tuko tayari kwa mashindano. Nadhani maandalizi ndiyo kitu kikubwa, tutacheza mechi mbalimbali za kirafiki ili kujiweka sawa," alisema kocha huyo.

Alisema michuano hii itakuwa na faida kwa sababu itachukua timu mbili za juu kwa ajili ya kufuzu AFCON na si kama ile ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia ambapo ilikuwa inatafuta mshindi mmoja tu wa kundi.

"Tofauti ya michuano hii ni kwamba zinafuzu timu mbili za juu kwa hiyo ni faida kwetu, hii ni tofauti ya ile ya kufuzu Kombe la Dunia ambapo timu moja tu ndiyo ilikuwa inasonga mbele," alisema Paulsen.

# *Simba yamburuza kocha Orlando CAF*

## Ala 'misumari' ya moto ndani nje, ni wakati ikipania kufanya maajabu Sauzi, yaomba...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wawakilishi pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba wakiendelea na maandalizi makubwa kuelekea mechi ya mkondo wa pili ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika ugenini dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini, uongozi wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao, umesema katu hautavumilia kashfa zilizotolewa na kocha wa wapinzani wao hao, Mandla Ncikazi.

**Jumapili wiki hii Simba inatarajia kushuka dimbani nchini Afrika Kusini kwenye mechi hiyo ya mkondo wa pili dhidi ya Orlando Pirates, ikiwa na faida ya bao 1-0 ililolipata katika mechi ya awali iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili iliyopita.**

Katika mechi hiyo Kocha wa Orlando, Ncikazi, alitoa shutuma nyingi dhidi ya Simba baada ya kupoteza mchezo huo, akidai timu yake kupata mapokezi mabovu, huku pia akiilaumu kwa kushinda kwa mgongo wa waamuzi.

Hata hivyo, Ncikazi alipata mapokeo tofauti kwa mashabiki wa Orlando nchini Afrika Kusini, wengi wakiponda uwezo wake mdogo wa kuifundisha timu hiyo na kuutaka uongozi wa timu hiyo kumtimua yeye na kocha mwenza, Fadlu Davids.

Pamoja na 'misumari' hiyo ya moto ambayo Ncikazi anaipata kutoka kwa mashabiki wa Orlando, uongozi wa Simba umekemea vikali kauli zake na kueleza kusikitishwa kwani si za kiunamichezo na ni kinyume na kaulimbiu ya mchezo wa kiungwana (Fair Play), huku ukiweka wazi dhamira yake ya kulifikisha suala hilo kwa wenye dhamana ya mashindano hayo, Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Simba imechukizwa na maneno ya kashfa yaliyotolewa na Kocha Ncikazi ambayo yanatanabaisha ukosefu wa taaluma na ukiukwaji wa maadili katika kazi yake ya ukocha, ambayo yanakinzana na ukweli ambao Simba tumekua tukiiushi kwa kutoa huduma bora kwa wageni wote wanaokuja kucheza nasi hapa Tanzania.

"Simba tulishangazwa na vitendo vya Orlando tangu kuwasili kwao Tanzania ambapo kama wenyeji tuliandaa mazingira yote rafiki kwa ajili yao ikiwamo usafiri wa basi kubwa, na gari ndogo lakini kwa sababu zao walikataa kutumia huduma tulizowaandalia," ilieleza taarifa hiyo iliyosainiwa na Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez.

"Vilevile tuliwashauri kukaa hoteli ya karibu na mji, lakini kwa matakwa yao walichagua kukaa nje ya mji ambapo ni mbali na uwanjani hali iliyosababisha kuchelewa mazoezi kwa zaidi ya saa moja, lakini pamoja na hayo maofisa wa Uwanja wa Benjamin Mkapa waliwaruhusu kufanya mazoezi licha ya kuwa muda kikanuni kwa timu kufanya mazoezi ulishamalizika. Ajabu ni kwamba Kocha Ncikazi hayaoni yote haya na kuamua kuipaka matope klabu yetu ambayo tunajivunia ukarimu na uungwaana kwa wageni wetu wote."

Aidha, ilieleza kuwa katika kile kinachoonekana kuwa Orlando walidhamiria kufanya vurugu Tanzania siku ya mchezo huo, waligoma kutumia mlango rasmi wa kuingilia vyumba vya kubadilishia nguo na badala yake wakatumia mlango wa kuingilia chumba cha mikutano cha wanahabari ambapo kiuhalisia si tabia ya timu kubwa.

"Kufuatia kashfa hizo zilizotolewa na Ncikazi, klabu ya Simba itawasilisha malalamiko rasmi kwenda kwa Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) na kupitia balozi za nchi zote mbili kuelezea yale yote yaliyoelezwa na kocha huyo.

"Katika nyakati hizi ambazo tunajiandaa na mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Aprili 24 ,mwaka huu, tunaiomba Serikali ya Tanzania na Serikali ya Afrika Kusini kutupatia ulinzi tukiwa safarini na tukiwa Afrika Kusini," ilieleza.

Aidha, Simba imekumbushia uhusiano mzuri wa kihistoria kati ya Afrika Kusini na Tanzania tangu enzi za ubaguzi wa rangi nchini kwao ambapo Tanzania ilikuwa sehemu ya kuwasaidia wapigania uhuru wa nchi hiyo kupambana na udhalimu waliokua wanafanyiwa watu wa Afrika Kusini, jambo ambalo kwa kashfa za Ncikazi zinaonesha wazi kuwa hajui lolote kuhusu uhusiano chanya uliopo baina ya pande hizi mbili.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >